

# UKOMBOZI KATIKA UKAMILIFU, KATIKA FURAHA



Nina furaha usiku wa leo, tena, kuwasalimu katika Jina la Bwana wetu mpendwa Yesu, Mwana wa Mungu aliyefufuka. Na Uwepo Wake ulikuwa tayari uko hapa nilipoingia, kwa hivyo tunatazamia kuona mambo ya ajabu mno, kwa wingi, “kuliko yote tuyaambayo au tuyawazayo,” usiku wa leo, ambayo Mungu atatumwagia, ya baraka Zake, na kumtukuza Yesu Kristo katikati yetu.

<sup>2</sup> Nilikuwa nikizungumza siku mbili zilizopita usiku... Jumapili usiku nafikiri tulikuwa na ibada ya uponyaji, na Jumatatu usiku nilikuwa nikihubiri. Kisha nikatoa... Nikaanzisha somo fulani, Jumapili asubuhi, huko maskanini. Nami nikawaza, tulipokuwa tuingojea umati wa watu uongezeke kidogo, kidogo ningeonyesha hisia zangu. Mimi...

<sup>3</sup> Moja ya siku hizi, Mungu akipenda, na atanisaidia, ningependa tu kuwa na kampeni kadhaa mahali hu—huna... kuingia tu na kuhubiri au kufundisha Maandiko, na kufanya wito wa madhabahuni, na kushuka madhabahuni na kuwaombea watu, na kama vile sisi Wabaptisti wa mtindo wa kale tulivyozeoa kufanya. [Mtu fulani anasema, “Amina.”—Mh.] Ni Wabaptisti wawili tu nimewasikia wakisema, “Amina.” Kwa hiyo kwani nyote mko wapi, usiku wa leo?

Mtu fulani alisema, “Ndugu Branham, kwani ulikuwa Mbaptisti?”

Kasema, “Naam,” nikasema.

<sup>4</sup> Nilikuwa nikihubiri hapa Arkansas, wakati mmoja. Jamaa fulani, mzee, akaponywa. Alikuwa... walikuwa... Alikuwa Mnazarayo. Alibeba magongo yake mgongoni, kesho yake, akizunguka mjini, akiwa na ma—maandishi juu yake, “Mungu alinitoa kwenye haya, jana usiku.” Na amelemaa kabisa. Ilikuwa huko Little Rock. Naye alikuwa hivyo kwa miaka kadhaa. Na kila mtu alimjua, kwa sababu alizunguka huku na huku, na alikuwa ameilaza chini kofia yake, na kuuza penseli kutoka kwenye hiyo kofia. Na kila mtu alimjua, kwa hiyo ilianza tu, ilifanya jambo kuu mjini.

<sup>5</sup> Na siku kadhaa baadaye usiku, nilikuwa nikihubiri, na—naye akasimama. Akasema, “Hebu kidogo, Ndugu Branham, hivi ungejali nikikuuliza jambo fulani?”

Nikasema, “La, bwana.”

<sup>6</sup> Naye akasema, “Vema,” akasema, “ni—nilipokusikia ukihubiri, nilijua wewe ni Mnazarayo.” Akasema, “Ndipo nikawaona Wapentekoste wote hapa, ndipo mtu fulani akaniambia wewe ni Mpentekoste.” Akasema, “Nilikusikia ukisema, muda mfupi uliopita, ulikuwa Mbaptisti.” Akasema, “Sielewi hili.”

<sup>7</sup> Nikasema, “Vema, hiyo ni rahisi. Mimi ni Mnazarayo Mbaptisti wa Kipentekoste.” Hiyo ni kweli. Hiyo ni kweli. Sisi tu... amini.

<sup>8</sup> Loo, marafiki, mimi si mfuasi wa kanisa lolote la kimadhehebu, na hata hivyo mimi ni mfuasi wa kila moja yao. Nilipoanza hii, nilisema, “Kristo ndiye kichwa changu. Biblia hii ndiyo kitabu changu cha kiada. Nao ulimwengu ndio kanisa langu.” Kwa hiyo, hivyo—hivyo ndivyo ninavyotaka kuwa mpaka nitakapokufa.

<sup>9</sup> Sasa, baada ya siku moja au mbili usiku, tutajaribu kuanzisha ibada ya uponyaji tena, tutakapopata... Bila shaka, nikiona vitanda hivi na machela zimewekwa hapa, ningependa kuona jambo fulani. Nina hamu sana ya jambo fulani kutendeka hapa Louisville, Kentucky, kwa sababu hili ndilo jimbo langu la nyumbani.

<sup>10</sup> Sijawahi kufanya ninii mzuri, kile mnachokiita mkutano mzuri, katika Kentucky. Wala sisemi hili kwa kukashifu hata kidogo. Ni—nimekuwa na mingi mibaya sana, sehemu nyingi. Lakini, ninamaanisha, papa hapa nyumbani kwangu mwenyewe, ni vigumu sana. Ni... ni vigumu sana kuvunja hilo. Sijui ni kwa nini. Lakini nadhani ni kwa sababu Yesu alisema, “Katika nchi yako mwenyewe,” na jinsi ingekuwa, hivyo labda ndivyo i—ilivyo. Lakini kamwe hatuoni miujiza mingi mno ya ajabu.

<sup>11</sup> Nilikuwa na ibada hapa, yapata mwaka mmoja ama miwili iliyopita, huko Jeffersonville, lakini ilitokea kwamba huyo mwanamke alikuwa ametoka hapa Kentucky mahali fulani. Alikuwa amegeuka chaki, kitu kama hicho, kutoka miguuni mwake kwenda chini; kuanzia kiunoni kwenda miguuni mwake, hasa. Naye ha—hakuwa ametembea, kwa miaka kumi na saba. Wengi wenu mlikuwako usiku huo, na mnakumbuka kisa hicho. Naye akasimama moja kwa moja na kutoka nje ya maskani, kama kawaida.

<sup>12</sup> Sasa, ningependa jambo fulani lianze hapa Louisville, ambapo ningeweza kuona uamsho wa mtindo wa kale ukienea katika jiji hili kubwa la kupendeza.

<sup>13</sup> Ni mji kama miji mingine yote; ni mwovu kama yote itokeavyo. Mnajua hiyo ni kweli. Siumizi Kentucky; maana, mimi ni Mkentak, pia. Vema. Lakini ni—ni kweli. Ni mwovu. Huu ndio maskani ya wiski yote na viwanda vya kutengeneza pombe, na vifaa viovu na kadhalika, hivyo, vinaendelea moja

kwa moja Louisville, Kentucky hapa, kwa hiyo huu ndio kiti cha Shetani.

<sup>14</sup> Lakini tunaweza kukivunja vipande vipande kwa Injili ya Yesu Kristo, kama sote tutakusanyika pamoja. Hiyo ni kweli. Inatupasa kuunganisha nguvu zetu pamoja na kusukuma.

<sup>15</sup> Wakati fulani uliopita, mwinjilisti mashuhuri sana nchini alikuwa, alisema, akizungumza juu ya huduma hapa. Alisema, “Vema, ukweli wa mambo ndio huu.” Akasema, “Ninapoingia mjini, kila kitu kote nchini hakina budi kuifadhili mikutano yangu la sivyo sitaenda. Hiyo ni kweli. Vema, hebu wazienu tu. Nafikiri labda kuna makanisa makubwa sitini au sabini ya Kibaptisti mumu humu Louisville. Mnaona? Vipi kuhusu Methodisti? Na ni mji wa Kimethodisti; Asbury ikiwa hapa juu. Mtu huyo angekuwa na nini kama angekuja katika mji huu, kwa Wamethodisti na Wabaptisti tu, achana na Wapresbiteri na wote?”

<sup>16</sup> Sasa ni makanisa mangapi ya full-Gospel yaliyomo humu mjini? Misheni mbili au tatu ndogo huku chini mahali fulani, makanisa madogo tu, hapa na pale, nayo yanashambuliana wao kwa wao.

<sup>17</sup> Kwa hiyo unapoingia, inakubidi kusimama kwa nguvu za huduma yako. Hiyo ni kweli. Na hata . . . kila mtu ni kama siasa zinaingia. Inategenea nguvu za huduma yako, kuvuta kutoka kwa chochote Bwana atakachotuma. Nalipenda hivyo. Ndugu, kama Yesu Kristo siye nanga yangu hapa, na tegemeo langu, basi sina kitu kingine cha kutegemea. Hiyo ni kweli. Yeye . . . Juu ya Kristo, Mwamba wenye imara, nasimama; sakafu zingine zote ni mchanga udidimiao, kwangu mimi. Afadhali niwahubirie watu watano ambao ninajua Mungu alikuwa amewatuma kusikiliza Ujumbe, kuliko kuwahubiria elfu kumi waliovutwa kwake kisiasa. Hiyo ni kweli.

<sup>18</sup> Afadhali nione wongofu mmoja wa mtindo wa kale, ashuke madhabahuni na kulia na kuomboleza sana, kuliko kuona watu elfu kumi wamesimama, kusema tu, “Vema, nitajaribu.” Ati kuijaribu? Yeye si Kristo wa kujaribu. Yeye ni Mtu wa kukubaliwa. Uishi au ufe, udidimie au uzame, mchukue Yeye kwa vyovyote vile. Hiyo ni kweli.

<sup>19</sup> Nikiomba, nikiwaombea watu elfu kumi usiku wa leo, nao wote wakafa asubuhi; kesho usiku ningerudi hapa nikiwaombea wagonjwa, nikiamini Neno la Mungu lilikuwa ni la kweli. Hiyo ni kweli.

<sup>20</sup> Kama nilikuwa nikifa; na watu elfu tano walikufa miaka mia moja iliyopita, na walikuwa katika Umilele muda mrefu hivyo, wakafufuka wakaja duniani, na kusema, “Ndugu Branham, usiliamini. Yeye si wa kweli. Usiliamini. Sisi—sisi tulimwamini, tukaenda; tumeshindwa.”

21 Bado ningesema, “Acha nife katika Yesu Kristo.” Hiyo ni kweli. Ninamwamini. Na huo ni moyo wangu wote, kila kitu kimewekwa sawa katika Hilo. Nami ninaliamini kwa moyo wangu wote, nami namtegemea Yeye.

22 Nami nawapenda watu Wake. Ninawapenda ninyi, raia wenzangu wa Ufalme wa Mungu. Nami nataka kusimama bega kwa bega pamoja nanyi, na kuubeba mzigo.

23 Sasa, usiku wa leo; nilitangaza, jana usiku, nilikuwa nizungumze kwa muda kidogo usiku wa leo, Bwana akipenda. Sitaki kuwaweka muda mrefu sana, kuwachosha, kwa sababu tunatarajia. . .

24 Nina kitu kama ngozi ya kondoo mbele za Bwana kwa ajili ya mkutano huu. Nami ninamtarajia Mungu afanye jambo litakalouendeleza mkutano papa hapa jijini. Ninyi ombeni, tekelezeni sehemu yenu; basi, Hukumu itakapokuja, sote tunaweza kusimama na kusema tulitekeleza sehemu yetu.

25 Katika mlango wa 20 wa Kutoka, na kuanzia kifungu cha 7, natamani kuzungumza kwa dakika chache tu, Mungu akiruhusu, juu ya ninii sana. . . vema, ningesema, sio somo bora sana, bali so—somo zuri. Jumapili iliyopita, kwenye shule ya Jumapili maskanini huko Jeffersonville, tulianza, juu ya, “ukombozi kwa Damu.”

26 Na hiki ndicho ninachojaribu kufanya, ikiwa unataka kujua kwa nini ninafanya hivi hapa. Wengi wenu mnasema hamjaniona nikihubiri katika uamsho wa uponyaji, lakini ni kwa kusudi fulani. Nafikiri, kama ningeweza kuwafanya watu wavunjike na kuja madhabahuni, basi ningepata kibali kwa Mungu kwa ajili ya Louisville, hiyo ni kweli, wakati watu kweli wanaposhuka mbele za Mungu na kuomba.

27 Na, basi, kuna wengi wenu, marafiki, ambao mnaomba, mnafunga, na mnaogopa kushika kile mnachokiomba. Hiyo ni kweli. Mnaona? Vema, haitakufaa kitu kufunga na kuomba, isipokuwa uwe na matendo ya kuendana nako. Imani yako yote, kwa hali yoyote, haitakufaa kitu isipokuwa toke moja kwa moja huko nje, na kukifuatilia kwa dhati, na kukichukua. Ni hayo tu. Unapaswa kwenda mbele. Huna budi kujitokeza moja kwa moja na kufanya jambo hilo, kwa vyovyote vile. Unapomba chochote, nenda ukakichukue. Mungu alisema ni chako, kwa hivyo usichukue chochote pungufu. Pata ulichoomba. Fanya hivyo, uone jinsi litakavyotokea. Naam. Usi—usirudi nyuma na kusema, “Vema, nitachukua cha pili.”

28 Nitachukua cha kwanza. Mungu aliniahidi, cha kwanza, hicho ndicho ninachotaka. Na kwa miaka hii ishirini na mitatu niliyomtumikia, amenipa mahali hapo. Nami. . . Na maadamu ninamwamini na kumpenda, Naye ananipenda, itakuwa hivyo tu kwa sababu Yeye anawajibika kwa Neno Lake. “Chochote utakacho, ukiomba, amini kuwa umekipokea, kitakuwa chako.”

Hivyo ndivyo alivyosema. Hiyo ni kweli? [Kusanyiko linasema, “Amina.”—Mh.] Hilo ni zuri. Vema.

<sup>29</sup> Napenda kuwasikia mkisema, “Amina.” Unajua, Dada Hoover, *amina* inamaanisha “iwe hivyo,” kwangu, unajua. Nami ni—nikianza kuongea, nisisikie mtu akisema “amina,” ni—ninachanganyikiwa kabisa.

<sup>30</sup> Hapa siku moja nilikuwa nikihubiri katika kanisa dogo, na—nami nilikuwa tu... Loo, sina adabu nyingi sana za mimbarani, kulingana na, nadhani, theolojia ya siku hizi, kwa hiyo nafikiri nikawa mtukutu kidogo. Nami nafikiri niliruka nikaketi juu ya mimbara, namna *hiyo*, na kunyakua kipaza sauti kwa mkono wangu, na kuketi pale, huku miguu yangu ikining’inia, nikihubiri kwa bidii nilivyoweza. Nikajirudia; sikujua nilichokuwa nikifanya. Baada ya dakika chache, nikapotea tena, ndipo nikajikuta chini katikati ya marefu ya kanisa, nikikunja miguu yangu ya suruali. Sijui kwa nini, lakini kwa kweli nilikuwa... Ningalipenda kukaa hapo kwa muda. Hilo ni jambo moja ningependa kusema. Ilikuwa ni mahali fulani ambapo hakika nilikuwa najifurahisha. Nilipaishia tu kwa siku kadhaa baadaye.

<sup>31</sup> Kulikuwa na mtu aliyenijia, naye akasema, “Aisee,” akasema, “unawezaje kuhubiri, na watu hao wote wakisema, ‘Amina?’”

Nikasema, “Hizo ndizo zinazonifanya kuhubiri.” Naam.

<sup>32</sup> Niliikuwa na mbwa mzee. Niliwinda kuuni. Nadhani nina marafiki wengi wa Kentucky hapa ambao wanapenda kuwinda kuuni. Kwa hiyo... Naye angekimbiza chochote kilichokuwako, na aende akipate, isipokuwa kicheche; naye hangejishughulisha kabisa na huyo. Sasa, angemkimbiza aingie chini ya kichaka kinene. Na jambo pekee nililopaswa kufanya, sikutaka kumfuatilia kule chini, nilikuwa na hakika. Kwa hiyo jambo pekee ningefanya, ni kuinua tu kile kichaka, na kumpigapiga na kupaza sauti, “Kamata, jamani! Kamata!” Naye angeenda kumkamata huyo kicheche.

<sup>33</sup> Sasa kicheche mbaya zaidi nimjuaye ni ibilisi. Na ukitaka kupapasa kidogo, paza tu sauti “amina” mara moja moja. Na mimi—mimi... Tutamsukumia mitini, baada ya kitambo kidogo, kisha twende tukamkamate. Mnaona?

<sup>34</sup> Mnajua, mzee Buddy Robinson, wengi wenu mmesikia habari zake. Sivyo? Kanisa la Nazarayo. Alisema, “Bwana,” kasema, “nipe uti wa mgongo kama msumeno wa magogo. Nipe maarifa mengi nchani mwa nafsi yangu. Na unijalie kupigana na ibilisi mradi tu nina jino moja, kisha nimuume kwa ufizi mpaka nife.” Nafikiri hilo ni zuri... Na hivyo ndivyo alivyofanya hasa. Hivyo ndivyo alivyofanya hasa; mzee sana, karibu umri wa miaka mia moja, na bado anahubiri Injili.

<sup>35</sup> Ninawasikia hao askari wastaafu wa kale wakihubiri namna hiyo. Hivi majuzi, ilitokea niliifungua redio, na ndugu mmoja mzee, jina lake Mordekai F. Ham, karibu na umri wa miaka mia moja, angali anahubiri Injili. Nikasema, “Mungu, mbariki, na jalia atiwe nyota katika taji yake atakapofika Huko.” Ndugu Ham, namfahamu kidogo tu. Moja ya siku hizi nataka kukutana naye kabla hajavuka ng’ambo, ile Nchi. Na, kwa hiyo, anaweza kupeana mikono na watu wengi Kule. Ninajua atakuwa na watu wengi wa kupeana mikono nao atakapofika Kule, loo, kwa sababu amekuwa askari mkongwe.

<sup>36</sup> Bwana awabariki sasa. Na sasa, kabla hatujaingia katika Neno hili, hebu na tumwombe Mwandishi wake ashuke na kutufunulia Hilo.

<sup>37</sup> Baba yetu wa Mbinguni mwenye fadhili, tunakukaribia Wewe, usiku wa leo, katika Jina hilo la kupendeza na zuri la Mwanao, Yesu; tukiziungama dhambi zetu, kwamba hatustahili kulitaja Jina Lake takatifu. Kwa kuwa... Familia yote ya Mbinguni inaitwa “Yesu.” Familia yote duniani inaitwa “Yesu.” Na katika Jina hilo kila goti litapigwa, na kila ulimi utakiri Kwake, wawe ni wenye dhambi au watakatifu. Ndipo, tunaponena katika Jina Lake, jinsi tunavyopaswa kutetemeka mioyoni mwetu, kwa uchaji, tunapozungumza. Kwa hiyo tunaomba katika Jina Lake, kwa uchaji, ya kwamba Wewe utatujia usiku wa leo, Bwana.

<sup>38</sup> Tuko hapa katikati ya jiji kuu, lenye kila namna ya hila ambazo Shetani amewafungia watu sana, katika biashara zao, katika kucheza kwake kamari, na ukahaba, wiski, na sigara. Na, Ee Mungu, na wahudumu wengi, mimbarani, wanayaacha tu yapite kana kwamba ilikuwa ni moja tu ya mambo ya kawaida.

<sup>39</sup> Lakini, Mungu, tupe sauti ya maonyo, tupate kuihubiri Injili moja kwa moja na kweli, tuweke shoka kwenye shina la mti, acha vibanzi vianguke popote pale. Lakini tusaidie, Bwana, kutangaza hukumu juu ya mambo kama hayo, na kuhubiri Injili ya Mwanao mpendwa, Yesu.

<sup>40</sup> Mungu, jalia jambo fulani litendeke ambalo litautikisa mji huu kwa ajili ya Ufalme wa Mungu. Kwamba, hata makanisa, ambayo yanaendelea tu pembeni, yakiwa na washirika wachache, Ee Mungu, jalia makanisa hayo yajae na kujaa pomoni na watu wema, wa mtindo wa kale, watakatifu, waliozaliwa mara ya pili. Tujalie, Bwana. Na jalia tupokee uamsho, uamsho wa mtindo wa kale, uliotumwa na Mungu utakaotikisa tu kutoka upande mmoja wa jiji hadi mwingine, na kuondoa uchoyo wote. Ee Mungu, usitupe mkutano wa muda mrefu. Tupe uamsho utakaofunga vilabu vya pombe haramu, na utakaorekebisha mambo; na kuwafanya watu kuja, wakati kengele ya kanisa inapolia, na kumiminika madhabahuni na

kuomba kabla ya ujumbe wa mchungaji, na kuwa tayari. Mungu, tujalie.

<sup>41</sup> Sasa, usiku wa leo, huenda kukawa na wagonjwa hapa, Baba. Na tunapozungumza juu ya wagonjwa, ama kwa ajili ya wagonjwa, pia, Roho Mtakatifu na amponye kila mgonjwa humu jengoni. Mwokoe kila mwenye dhambi. Mwhite, nyumbani, kila aliyerudi nyuma kutoka kwenye njia yake potovu.

<sup>42</sup> Na sasa jalia Roho Mtakatifu awe Ndiye ambaye ameniongoza kwenye somo hili, usiku wa leo. Na jalia achukue mambo ya Mungu na amtumie tu mtumishi Wake hapa kama chombo, Mungu na apokee utukufu. Kwa kuwa tunaomba katika Jina Lake. Amina.

<sup>43</sup> Katika kifungu cha 7 cha mlango wa 20 wa—wa Hesabu, tunasoma hili.

*Kisha BWANA akasema na Musa, akamwambia,*

*Twaa ile fimbo, ukawakusanye mkutano, wewe na Haruni ndugu yako, . . . ukauambie mwamba mbele ya macho yao; nao utatoa maji yake, . . .*

<sup>44</sup> Nataka utambue hilo, maji “Yake.”

*. . . utatoa maji Yake, nawe utawatolea maji katika jabali: ndivyo utakavyowanywesha kusanyiko na wanyama wao.*

*Musa akaitwaa ile fimbo mbele ya BWANA, kama alivyomwagiza.*

*Musa na Haruni wakawakusanya makutano mbele ya mwamba, akawaambia, Sikieni. . . ninyi waasi; ni lazima tuwatokezee maji kwenye mwamba?*

*Musa akainua mkono wake, akaupiga ule mwamba kwa fimbo yake mara mbili: maji yakatoka kwa wingi, mkutano ukanywa, na wanyama wao pia.*

<sup>45</sup> Bwana na ayachukue Maneno haya machache sasa, tunaporudi kwenye somo letu la jana usiku na kulileta kwenye hili, Mungu akipenda.

<sup>46</sup> Na sasa, ninataka wagonjwa wote walio hapa ndani, usiku wa leo. . . Sasa, Billy kamwe hakusambaza kadi zozote za maombi leo, maana nilimwambia asitoe. Nilisema, “Nenda tu, Billy, ukamwambie Ndugu Cauble. Na hebu mimi tu. . .”

<sup>47</sup> Ninajaribu jambo fulani, kwa ajili ya utukufu wa Mungu. Kumwomba Mungu tu atusaidie, atupe watu katika Ufalme; na Waaminio watakaotia nguvu imani yao, na kupanda juu, hata bila kitu kingine chochote, watapanda tu na kusema, “Mungu, ninakuamini, juu ya Neno.” Ndivyo hivyo. Hiyo hapo njia ya asili, ya kwanza na bora zaidi. Hiyo ni kweli. Amini Neno la Mungu. Ndipo, kama huwezi kufanya hivyo, basi, bila shaka, Mungu anaingiza mambo mengine, kama vile karama

na ishara, ku—kulithibitisha Neno Lake, kulithibitisha kwa kila mwaminio.

Sasa, Jumapili, tulikuwa na, “ukombozi kwa Damu.”

<sup>48</sup> Tunawachukua Israeli sasa, katika safari yao, wakitoka Misri, mfano wa ulimwengu, wakienda zao Palestina, nchi ya ahadi. Nafikiri ni jambo zuri. Nalipenda tu. Karibu kila juma, mimi huketi na kusoma Kitabu hicho chote cha Kutoka, nikiweza, ama sehemu kubwa yake niwezayo. Ninakipenda kwa sababu ni mfano kamili wa kanisa siku hizi, hali yake, na jinsi Mungu anavyotenda kazi. Alivyotenda kazi wakati huo, yale aliyofanya katika mambo ya kawaida wakati huo, anatenda katika mambo ya kiroho sasa. Mnaiona?

<sup>49</sup> Sasa, hapo aliwaongoza Israeli, wa kawaida, ambapo waliona, wakatazama, akawahamisha kutoka katika nchi fulani na kuwaingiza katika nchi nyingine ya kimaumbile.

<sup>50</sup> Sasa tunaongozwa na Roho Mtakatifu, katika kuingia sasa katika Nchi ya ahadi. Mnaamini tuko njiani kwenda kwenye Nchi ya ahadi? [Kusanyiko linasema, “Amina.”—Mh.] “Nyumbani mwa Baba yangu mna makao mengi. Kama sivyo, ningewaambia. Nitaenda na kuwaandalia mahali.” Je, hiyo ni kweli? [“Amina.”] Sasa tuna Nchi ya ahadi ambayo tunaiendea, na kila siku inaashiria hatua muhimu; siku nyingine, hatua nyingine.

<sup>51</sup> Na kuna uvuli mkubwa wa giza umewekwa kule mbele zetu, unaoitwa mauti. Na kila wakati moyo wetu unapopiga, tunasonga hatua moja karibu zaidi na hiyo. Moja ya siku hizi, utapiga pigo lake la mwisho, ndipo tutaingia. Nataka kuwa kwenye wakati wangu, kuchukua kura yangu; kama ninavyotumaini kila mmoja wenu alivyo, usiku wa leo. Ninapojua ya kwamba iko mbele yangu, na sina budi kukutana nayo, sitaki kuwa mwoga. Nataka kujivika vazi la haki Yake, nikiingia ndani yake, nikijua jambo hili, ya kwamba nina hakika ya kwamba ninamjua katika Nguvu za kufufuka Kwake. Hiyo ni kweli. Kwamba, atakapoita kutoka kwa wafu, nitaitwa pamoja na hao walio hai. Mungu ni Mungu wa walio hai.

<sup>52</sup> Sasa, walipokuwa wakisafiri katika nchi hii, tuliona ya kwamba Mungu alifanya ninii—alifanya mpango kwa ajili yao. Alileta ukombozi, kwa damu. Ndipo tunaona, Yeye analeta ukombozi, tena, kwa nguvu.

<sup>53</sup> Tuliona, majuzi usiku, ya kwamba Yeye aliagiza damu ipakwe; ambayo ilikuwa ni mfano mzuri sana wa mwaminio, kwamba, wakati amekubali kifo cha Kristo badala yake, basi anafanyika mtoto wa Mungu. Anaanza safari yake.

<sup>54</sup> Sasa, jambo lingine analopaswa kuwa nalo...baada ya kuokolewa, kiroho.

55 Sasa, kifo cha mwana-kondoo asiye na hatia kilitoa uhai kwa mwaminio mwenye hatia. Je, huo si ni mfano mkamilifu sasa? Kifo cha Asiye na hatia, akitoa Uhai kwa ajili ya wenye hatia. Nacho kifo cha Kristo asiye na hatia hutoa Uzima kwetu sisi wenye hatia.

56 Sasa, kwanza, basi, baada ya Mungu kuwapa uzima kwa njia ya damu, na kuthibitisha, ya kwamba mauti ilipita juu yao, Yeye aliwafanya kuanza katika safari yao. Tutawafikia baada ya muda mfupi.

57 Sasa angalieni, basi, jambo lingine ambalo Mungu alifanya, mara tu walipofanyika waaminio na watoto, na kumkubali Mungu, adui wa mauti ya kimwili aliwafuatilia. Naye akawazingira, moja kwa moja; na jangwa upande mmoja; Bahari ya Shamu upande huo mwingine; milima upande mwingine; Jeshi la Farao likija, likiwafuatilia, mamilioni ya askari wakija taratibu, kuwashinda.

58 Sasa, Mungu alikuwa amedhihirisha ya kwamba alikuwa amewapa uzima, kupitia kifo cha mwana-kondoo; sasa atawaonyesha ukombozi wa kimwili. Haleluya! Mnaona, kwa ajili ya wokovu na uponyaji pia, mnaona, kwa ajili ya mtu wa kawaida na wa kiroho.

59 Malaika wa mauti alipitia juu, ikithibitisha kwamba Mungu alikuwa ameandaa njia ya kuepukia, kupitia toleo la hiyo damu, nao wakaikubali. Sasa Yeye atafanya njia ya kuepukia mauti ya kimwili.

60 Kama vile mwaminio, mara tu anapookoka. Labda kansa imemla, au ugonjwa fulani. Mungu anao ukombozi, pia, kupitia kwa nguvu. Sawasawa na alivyo na ukombozi kwa ajili ya nafsi, anao ukombozi kwa ajili ya mwili. Ilikuwa ni . . .

61 Walikuwa wameokoka, na wametahiriwa. Walikuwa chini ya damu, lakini, hata hivyo, Farao alikuwa anataka. . . . Adui alikuwa anataka kuwaangamiza, kuwaua wote pale pale nyikani, ndipo Mungu akaonyesha nguvu zake za ukombozi kwa ajili ya mwili wao. Mnalipata? Mnajua ninachozungumzia? [Kusanyiko linasema, "Amina."—Mh.] Ukombozi kwa nguvu! Na basi, wakati adui alipokuwa papo hapo karibu kuwakamata, ile Nguzo kuu ya Moto ya kimbinguni ikatoka juu ya Israeli, ikaja hapa na kusimama kati yao na mauti.

62 Acha lizame kwa dakika chache. Je, mnaweza kuona ninachozungumzia? [Kusanyiko linasema, "Amina."—Mh.]

63 Sasa, kwa kila mwaminio, mtoto wa Mungu aliyezaliwa mara ya pili, kifo kinapokuja mlangoni kuiba, kabla ya wakati wake, Malaika wa Mungu anasimama kati yako na huo ugonjwa. Sasa, kama ukitaka kuendelea nao, hiyo ni shauri yako; lakini sio lazima uendelee nao. Unaona? Amesimama kati yako na mauti.

<sup>64</sup> Miaka ishirini na mitatu iliyopita, katika Hospitali ya Kiyahudi, Dk. Morris Fletcher alinipa saa tatu; mmoja wa madaktari wenu wa upasuaji walio bora sana hapa mjini, alinipa saa tatu za kuishi. Ninaishi, usiku wa leo. Haleluya! Kwa nini? Kwa neema isiyostahiliwa, Malaika wa Mungu alisimama kati yangu na mauti, kunilinda, nami nikaukubali. Na katika shukrani, kwa neema ya Mungu, nimemletea watu nusu milioni, usiku wa leo.

<sup>65</sup> Loo, jinsi Mungu anavyojua jinsi ya kufanya mambo, kama tu tutafuata. Usijaribu kumwongoza Mungu. Acha Mungu akuongoze. Unaona? Sisi ndio wa kuongozwa. Nafikiri ndiyo maana Mungu alitufananisha na kondoo.

<sup>66</sup> Je, umewahi kumwona kondoo akiwa amepotea? Mbona, yeye ndiye kiumbe asiyejiweza zaidi duniani. Hawezi kupata njia yake popote. Yeye husimama tu na kulia mpaka mbwa mwitu anamla, ama anafia pale. Hawezi kupata njia yake ya kurudi.

<sup>67</sup> Na hivyo ndivyo, kwamba, mtu anapopotea, hajiwezi kabisa. Hakuna unachoweza kufanya juu yake. Mungu, kwa njia ya neema, hana budi kukuongoza kwa Kristo. Yesu alisema, “Hakuna mtu awezaye kuja Kwangu asipovutwa na Baba. Na wote anaowavuta, na wajao, nitampa Uzima wa milele.” Ni ahadi iliyoje!

<sup>68</sup> Loo, laiti ningaliweza kumleta kila mtu humu, ambapo lingezama chini kabisa chini ya ubavu wa tano upande wa kushoto, mpaka likagonge kiini cha moyo. Ungewaona watu wakisimama tu, huku kila namna ya magonjwa yakining’inia juu yao, wakitoka nje ya jengo hili, wakishangilia, wakikataa kuwa nayo. Viwete wangetembea kawaida kadiri wawezavyo. Wangekataa kujua kitu kingine chochote. Unaona?

<sup>69</sup> Unaogopa. Unaogopa kuanza. Unamsubiri Mungu ashuke na kukuvuta nje. Mungu halifanyi hivyo. Wewe ndiye unayepaswa kuchukua hatua. Anatoa ahadi, na kusema, “Njoo,” halafu unafuata.

<sup>70</sup> Sasa waangalieni wana wa Israeli, basi. Mungu alikuja na kusimama kati yao na hatari; nguvu za ukombozi. . . ukombozi kwa nguvu, hasa. Ukombozi kwa damu; ukombozi kwa nguvu.

<sup>71</sup> Jana usiku tuliwaacha, wakitambaa tu ukingoni, upande wa pili wa Bahari ya Shamu. Adui wote, magurudumu ya magari yao yalikuwa yameng’olewa. Farasi wao walichanganyikiwa, pale katikati ya mto, nao walikuwa wakigeuka kila upande, wakienda *huku*, na magurudumu yamezama matopeni na kuchomoka. Na kundi la watu likikimbia kiwazimu, adui. Ndipo Israeli wakapanda ukingoni, kumwona Mungu akinyosha mkono Wake na kuwaangamiza adui wote.

<sup>72</sup> Mfano mzuri, mwaminio, chini ya Damu; alikuwa ameponywa basi na mpatanishi, nguvu za Mungu zikiyahifadhi

maisha yake, kuyarefusha kwa muda. Wangeliuawa, kila mmoja, papo hapo; angewaua kinyama mumo humo nyikani, kama Mungu hakusimama kati yao. Ningelikuwa nimekufa, muda mrefu uliopita, kama Mungu asingelisimama kati yangu na mauti. Kila mwaminio humu ndani angekuwa amekufa, muda mrefu uliopita, kama Mungu hakuwa amesimama kati yako na mauti; kila mmoja wenu. Kwa hiyo, Mungu, katika neema Yake kuu na rehema, anasimama kati ya mwaminio na mauti. Haleluya!

<sup>73</sup> Hii hapa. Basi ni jambo gani linalofuata kwa mwaminio? Jambo linalofuata ni ubatizo wa Roho Mtakatifu basi. Musa aliwaongoza wana wa Israeli moja kwa moja hadi kwenye Bahari ya Shamu, wakabatizwa katika Bahari ya Shamu. Bahari, maji, yakiwakilisha Roho. Alipoupiga ule Mwamba, maji yalitokea. Nayo yalikuwa ni mfano wa Kristo, katika Yohana 3:16. “Mungu aliupenda sana ulimwengu, akamtoa Mwanawe wa pekee, ili kila amwaminiye asipotee, bali awe na Uzima wa milele.” Angalieni, watu waliokuwa wanaangamia, nyikani, waliokolewa na Mwamba uliopigwa. Nao watu wanaoangamia wanaokolewa siku hizi (wanaoangamia katika dhambi, wanaoangamia katika uovu) kwa sababu Mwana wa Mungu aliyepigwa alipachukua mahali pao; maji, Roho, akitiririka!

<sup>74</sup> Angalieni, ninawatakeni mlione sasa, walipokuwa wakipitia kwenye Bahari ya Shamu, ilikuwa ni mfano wa kumpokea Roho Mtakatifu. Baada ya mwaminio kukombolewa kutoka katika mauti, kuingia Uzimani; nguvu za Mungu zimeuponya mwili wake; sasa yeye ni mtaradhiwa wa ubatizo wa Roho Mtakatifu. Sasa yeye ana safari, kule, mbele zake; lakini, kabla hajakabiliana na safari hiyo, hana budi kuwa na kitu cha kumvusha. Amina. Mfano kamili wa Pentekoste!

<sup>75</sup> Angalieni, walipokuwa wakitambaa kutoka ufukoni. Kila mwaminio, unapoingia na kuokolewa, kuikubali Damu ya Yesu, ungali unajaribu kushikilia *hiki* na kushikilia *kile*, wala huwezi kuacha *hiki* na huwezi kuacha *kile*. Baada ya kitambo kidogo, huenda Mungu akakutendea mema; lakini huwezi kuacha sigara zako, inakubidi kunywa kileo na wenzako mara kwa mara. Lakini unachohitaji kufanya ni kupita kwenye Bahari ya Shamu.

<sup>76</sup> Wakati walipofika ng'ambo ya pili. Hili hapa. Nataka mulione. Walipofika ng'ambo ya pili, walitambaa ukingoni na kutazama nyuma, na kuwaona maskini wale wanyapara wote waliokuwa wamewapiga, wakawaua baadhi yao. Kama vile tu kansa na sigara na tumbaku na wiski na kadhalika, vitiavyo watoto wazimu, vikawapeleka kwenye hospitali za wendawazimu, hospitalini, na kundi la waliochanganyikiwa na chochote kile kinachotolewa ulimwenguni. Walipotazama nyuma na kuona vitu hivyo vyote viking'ang'ana, havijiwezi,

na vinafia baharini. Ndugu, nena kuhusu mkutano; walikuwa na mmoja!

<sup>77</sup> Musa! Loo, nitaacha hili lizame kilindini. Natumaini litazama ndani kabisa. Musa, nabii mkuu sana aliyepata kuishi, nje ya Yesu Kristo. Kamwe hakukuwako na mtu ambaye Mungu aliwahi kuzungumza naye, kama alivyofanya Musa, nje ya Kristo. Alisema, “Kukiwako na mtu aliye wa kiroho, au nabii, kati yenu, nitamwonyesha maono na kujitambulisha Mwenyewe kwake. Lakini si mtumishi Wangu Musa; ninazungumza naye mdomo kwa sikio.” Hiyo ni kweli.

<sup>78</sup> Musa, mtu huyu muungwana. Mara tu alipopitia tukio hilo, aliwaona wanyapara hao wote wamekufa, alijua vitu hivyo vyote vilikuwa vimepita milele wakati huo. Vitu hivyo vyote ambavyo vilikuwa vimewasukuma, na kuwapiga, na kuwachapa viboko, vilikwisha. Aliinua mikono yake na kuimba katika Roho. Loo, jamani!

<sup>79</sup> Halijawahi kuwa na kifani, wala halitakuwa nacho, mpaka tufike Utukufuni kule juu. Utimilifu ulipokamilishwa pale, aliimba katika Roho. Na tunapokombolewa katika mwili . . .

<sup>80</sup> Huo ulikuwa ni mfano wa Roho Mtakatifu akija kwenye Pentekoste, tulipopitia baharini. Ilikuwa ni mfano wa Pentekoste. Naye Musa, katika mfa- . . .katika mfano kule nyuma, alipopitia hapo, aliimba katika Roho. Ilikuwa kwenye Siku ya Pentekoste. Nao mwili unapokuwa mkamilifu, umekombolewa . . .Sasa nafsi zetu zimekombolewa kikamilifu, kweli, “haziwezi kuangamia; zina Uzima wa milele.” Kile Biblia isemacho!

<sup>81</sup> Loo, najisikia vizuri. Angalia ni kwa nini. Kwa sababu ninajua ni BWANA ASEMA HIVI. Naitia tu nafsi yangu nanga pale, na kuendelea kutembea, na kusema, “Shetani, piga tu kelele utakavyo, kwangu mimi. Hainisumbui, maana ninamjua Yeye ambaye nimemwamini, nami nimesadiki ya kwamba anaweza kukilinda kile nilichoweka amana Kwake hata Siku ile.” Amina.

<sup>82</sup> Tunachohitaji usiku wa leo ni uamsho mzuri, wa mtindo wa kale, wa Billy Sunday, uliopondeka, wa kiroho, ndio tunaohitaji huku karibu na Louisville. Hiyo ni kweli, tunahitaji uamsho mzuri wa kipentekoste, wa mtindo wa kale, uliotumwa na Mungu. Naam, bwana.

<sup>83</sup> Angalia, basi, wakati miili yetu itakapokombolewa . . . Ambapo, tuna uponyaji wa Kiungu sasa, kama kivuli.

<sup>84</sup> Kama vile hicho kilivyokuwa ni kivuli pale cha Pentekoste, angalia walichofanya katika huo wakati wa kivuli, wa wokovu. Angalia jinsi walivyotembea kule mbele za Mungu, “Wakazima . . .makali na kadhalika . . .ya moto, na kuepuka makali ya upanga,” mambo haya yote waliyafanya, “wakatoka

katika tanuru za moto; mbali na tundu la simba, na kadhalika,” kwa kivuli, haleluya, kwa kivuli cha Pentekoste.

<sup>85</sup> Sasa tuna ukombozi mkamilifu kupitia Damu ya Kristo. Wasingeweza kuwa na ukombozi mkamilifu wakati huo, maana ilikuwa chini ya damu ya mafahali na mbuzi, wala haitaondoa dhambi; ilifunika tu dhambi. Lakini wakati Damu ya Yesu ilipomwagika, ile Damu takatifu sana yenye haki, dhambi hazikufunikwa tena; zilitalikiwa na kuondolewa mbali, naye mwaminio anaenda Mbele za Muumba wake. Haleluya!

<sup>86</sup> Kama walifanya hivyo wakati huo, kivuli pale, cha Musa akiimba katika Roho; basi, huko katika Ufunuo, wale walio na ukombozi mkamilifu wa mwili, walisimama juu ya bahari ya kioo na kuimba wimbo wa Musa tena, katika Kitabu cha Ufunuo.

<sup>87</sup> Ati kunena juu ya m—mkutano wa Roho Mtakatifu? Walikuwa nao waliposimama kwenye ufuko huo. Sikiliza, dada. Maskini Miriamu mwenye heshima, yule nabii mke, dada yake Musa, nabii mke, alisisimkwa sana mpaka akashika tari na kushuka mbio ukingoni, akipiga tari hii, na kucheza katika Roho. Si hivyo tu, bali binti wote wa Israeli walimfuata, wakicheza katika Roho. Kama huyo si Roho Mtakatifu akishuka, sijawahi kumwona mmoja. Mbona, bila shaka, hayo, mataifa hayo yote ya kitamaduni, yenye heshima yangeweza kutazama kupitia darubini zao na kuona kwamba, wangesema, “Ulokole.” Kweli. Lakini ilikuwa ni Mungu. Kweli!

<sup>88</sup> Mambo ya heshima yanadharau, siku hizi, wale ambao Mungu amewabariki. Kweli!

<sup>89</sup> Inanikumbusha hadithi moja. Jamaa fulani alikuwa na shamba kubwa zuri. Akajenga maghala makubwa mno mazuri, ya heshima tu na ya kipekee kadiri yalivyoweza kuwa, lakini alikuwa mvivu sana kulima. Vema. Kulikuwa na mkulima mwingine aliyeishi karibu naye; hakuwa na ghala zuri, lakini alikuwa ni mkulima kwelikweli, naye alikuwa ameweka vyakula vingi vizuri katika ghala lile mwaka ule. Ndipo ndama wawili wadogo wakazaliwa, mmoja katika kibanda kimoja na mwingine katika kingine. Majira ya kuchipua yalipowadia, waliwatoa hao ndama zizini.

<sup>90</sup> Maskini huyo ndama mdogo kutoka hapa, alikuwa amelishwa vizuri sana, jamani, wakati huo upepo ulipoanza kumpiga, loo, jamani, alirusha mateke yake, naye huyo akaondoka, mbio tu alivyoweza kwenda; akikoroma, na kurukaruka, na kupiga kelele, na kuendelea.

<sup>91</sup> Ndipo yule mkulima mwingine akamfungulia wake, kule. Hakuwa na—hakuwa na chakula ila magugu; mvivu sana kulima, mvivu sana kumlisha.

<sup>92</sup> Inanikumbusha juu ya baadhi hawa ya wachungaji. Kweli! Kweli! Wavivu sana! Wazembe sana. Na maghala ya heshima

ndiyo tu mliyo nayo. Mnaweka Chakula mle ndani kwa ajili ya ndama! Kweli. Kweli. Ubatizo wa Roho Mtakatifu, unaohubiriwa kwa nguvu, utayaunguza. Hiyo ni kweli. Lakini hicho ndicho wanachohitaji, ni kuunguzwa kuzuri kwa mtindo wa kale; kile kanisa linachohitaji, kile washiriki wanachohitaji. Angalieni.

<sup>93</sup> Naye maskini ndama huyu mdogo alikuwa ameharibiwa. Maskini, jamaa mdogo alipotoka kibandani, alikuwa amekonda sana alitembea kwa shida. Ndipo akachungulia chini ya ufa, na kutazama upande wa pili.

<sup>94</sup> Naye akamwona ndama huyo mwingine akikoroma tu. Alikuwa mnene na mduara. Alijisikia vizuri. Alikuwa akila msimu wote wa baridi kali.

<sup>95</sup> Ndipo ndama huyo mdogo, mwenye njaa akatazama, akasema, “Ulokole wa jinsi gani!” Jamani! Hakika, alikuwa amekonda sana kuwazia jambo lolote lingine.

<sup>96</sup> Lakini, ninawaambia, wakati yule ambaye alinenepa sana, msimu wote wa baridi kali, ndugu, alijua mahali alipokuwa. Alikuwa na wakati mzuri wakati huo upepo wenye joto ulipoanza kuvuma juu yake.

<sup>97</sup> Na mtu yeyote ambaye amezaliwa kwa Roho wa Mungu, watamwita mlakole ama chochote kile. Lakini wakati huo upepo wenye joto, wa masika, wa Roho Mtakatifu utakapoanza kuja kama ulivyofanya kwenye Siku ya Pentekoste, jambo fulani litatukia. Hakika. Upepo wenye joto ukaanza kuvuma; ndugu, nyote mmenenepa kwa Injili, pande zote na mnajisikia vizuri. Rusheni mateke yenu na mwe na wakati mzuri.

<sup>98</sup> Hivyo ndivyo Miriamu na wengineo walivyofanya. Waliangalia nyuma na kuona mambo hayo yote ya kale waliyofanya wakati mmoja, yote yalikuwa yamekufa na kutoweka. Walikuwa tayari wamemwona Mungu akiikubali ile damu; tayari walikuwa wameona nguvu Zake katika uponyaji wa Kiungu, zikisimama kati yao; wakitipia Bahari ya Shamu, nao wakabatizwa kwa Roho; wakatembea huo upande mwingine, wakiwa tu na wakati mzuri. Hawakujali kile ninii . . . mashirika yote yalichofikiria juu yake. Amina.

<sup>99</sup> Ni mfano mkamilifu jinsi gani siku hizi, wa mwaminio atakayethubutu kupiga hatua atoke nje.

<sup>100</sup> Mungu aliahidi kwamba angewapa kila wanachohitaji. Aliahidi atatupa kila tunachohitaji. Hakuwahi kuwaambia, “Nitafanya njia ya uponyaji; nitafanya njia ya *hii*; nitafanya njia ya *ile*.” Alisema, “Nitakuwa pamoja nanyi!” Haleluya!

<sup>101</sup> Hivyo ndivyo alivyotuambia. “Nitakuwa pamoja nanyi, hata ndani yenu, hata ukamilifu wa dahari.” Hilo ndilo tu ninalopaswa kusema. Haikubidi kubishania *hiki*, *kile*, au *kinginecho*. Ikiwa Yeye yuko hapa, hilo linaniridhisha; Uponyaji

wa Kiungu uko hapa, Nguvu ziko hapa. Kila kitu alichokuwa kule, ndicho alichosasa, “Yesu Kristo ni yeye yule jana, leo na hata milele.” Kwa hivyo, unaweza kuchukua theolojia yako na kuzama nayo. Ndugu, ninaamini Yesu Kristo yeye yule jana, leo, na hata milele; kasema, “Nitakuwa pamoja nanyi, hata ndani yenu, hata ukamilifu wa dahari.” Naam.

<sup>102</sup> Na hapo wakatoka, Naye alikuwa pamoja nao. Sasa alisema... Loo, walikuwa na kikapu kidogo cha mikate juu ya kichwa chao; wote ulikuwa umeliwa ukaisha. Hawakuwa na wowote. Wakaenda kulala, wakiwa na njaa kidogo usiku huo. Lakini asubuhi iliyofuata walipoamka, kulikuwako na mikate imetandaa kote ardhini.

<sup>103</sup> Hivyo ndivyo Mungu anavyofanya mambo; anakuacha ushuke chini hadi dakika ya mwisho, kisha akuonyeshe kile anachoweza kufanya kulihusu. Hiyo ni kweli. Anapenda kufanya hivyo. Anapenda. Anapenda kuwashangaza watu Wake.

<sup>104</sup> Wewe mwanaume unapenda kumfanyia mke wako hivyo. Unasubiri hadi siku yake ya kuzaliwa, unamweka tu chini ya matarajio, kwa sababu unampenda.

<sup>105</sup> Hiyo ndiyo sababu Mungu hutuacha tufike mwisho wa njia wakati mwingine, kwa sababu anatupenda na anataka kuthibitisha mambo Yake ya kimbinguni na nguvu Zake. Kwa sababu anatupenda, hiyo ndiyo sababu Yeye hufanya hivyo. Naam. Anatuacha tu tufike mahali ambapo tuko karibu tu kupiga hatua ya mwisho, ndipo anajitokeza jukwaani.

<sup>106</sup> Aliwaacha wale wana wa Kiebrania waingie moja kwa moja kwenye tanuru ya moto, lakini kulikuwako na Mtu wa nne amesimama pale na feni, akiwayoyoea. Mnaona? Yeye yuko kila wakati. Haondoki kamwe. Sikuzote Yeye yuko karibu. “Malaika wa Bwana hufanya kituo akiwazunguka wale wamchao.”

<sup>107</sup> Huko, usiku ule, waliokota mikate hiyo kesho yake asubuhi. Ninaweza kuwaona wale Waisraeli waliokuwa wamepitia katika Bahari ya Shamu hivi punde; walikuwa ndio kwanza wakombolewe kwa damu; wakazona Nguvu za Mungu za uponyaji, ama Nguvu za kimiujiza zikisimama kati ya Mungu... na kati ya Israeli na Misri; na zilikuwa zimewazamisha adui nyuma ya hapo.

<sup>108</sup> Kama vile kansa ya kale imekwisha milele, upofu ulikuwa umekwisha, uziwi umetoweka, kisukari kilikuwa kimekwisha, kila kitu tayari kimezamishwa kule nyuma katika Damu ya Yesu Kristo. Unajisikiaje? Jamani!

<sup>109</sup> Unatembea barabarani, na maskini mkosoaji fulani anasema, “Sasa ngoja kidogo! Una uhakika na hilo?”

“Usizungumze nami.” Amina. Loo, jamani!

<sup>110</sup> Ninaweza kuwaona huko nje, wakikusanyika tu na kukusanyika, na wakila, na kuwa na wakati mzuri sana. Ni

kama tu mkutano wa mtindo wa kale, wa Roho Mtakatifu. Hapa atakuja Roho wa Mungu akimwendea maskini mtakatifu fulani, atainua mikono; aingie moyoni namna hiyo, na kupiga mayowe, “Bwana asifiwe!” Mkutano tu wa mtindo wa kale namna hiyo. Naam, bwana. Walikuwa wakiikamata tu kutoka upande mmoja hadi mwingine, wakiwa na wakati mzuri.

<sup>111</sup> Sasa, mkate huo kamwe haukukoma. Uliendelea kote kote safarini, kwa ajili yao. Hiyo ni kweli. Na ilikuwa ni mfano mkamilifu wa pentekoste ndani yetu. Hiyo ilikuwa katika mambo ya kawaida. Mkate huo haukukoma kamwe. Ulidumu mkate ule ule, mpaka walipoingia katika nchi ya ahadi. Hiyo ni kweli? Ninyi wasomaji wa Biblia mnajua hilo. Ndipo wakati sisi. . .

<sup>112</sup> Kanisa lilizinduliwa katika Siku ya Pentekoste, wakati waaminio walipokuwa kule juu. “Kukaja uvumi kama upepo wa nguvu ukienda kasi, ukaijaza nyumba yote waliyokuwa wameketi.” Roho Mtakatifu yeye yule aliyeshuka wakati huo, anashuka sasa. Ataendelea moja kwa moja kutoka wakati huo hadi mwisho wa wakati. Ataendelea moja kwa moja. Ndiye mkate wetu. Walilishwa mkate wa kawaida; tunalishwa mkate wa kiroho.

<sup>113</sup> Yesu alisema, “Mimi ndimi Mkate wa Uzima utokao Mbinguni, kwa Mungu.”

<sup>114</sup> Walisema, “Baba zetu walikula mana nyikani, kwa muda wa miaka arobaini.”

Akasema, “Wamekufa, kila mmoja.” Naam, bwana.

<sup>115</sup> “Lakini yeye aulaye mwili Wangu na kuinywa Damu Yangu, yuna Uzima wa milele, nami nitamfufua katika siku za mwisho. Mimi ndimi Mkate wa Uzima unaotoka Mbinguni, kwa Mungu. Mtu akila Mkate huu, hatakufa kamwe.” Haya basi. Walikuwa na wa kawaida; tuna wa kiroho. Loo, nisingeubadilisha kwa chochote. Ajabu!

<sup>116</sup> “Loo,” unasema, “Ndugu Branham, sote tunajua wewe ni mlokole.” Vema, najua, pia. Mimi ni mpumbavu kwa ajili ya Kristo. Wewe ni mpumbavu wa nani? Huenda ikawa wewe ni mpumbavu wa ibilisi. Vema. Kwa hivyo, ni afadhali niwe mpumbavu kwa ajili ya Kristo, nanyi je? Vema.

<sup>117</sup> Angalieni, hili hapa jambo lingine kuhusu hiyo mana. Walipoanza kuionja, walisema, “Ina ladha ya asali.” Naam, ilikuwa tamu. Ninaweza tu kuwaona hao watakatifu wa kale wakijiramba midomo yao na kuila yote. Ilikuwa nzuri.

<sup>118</sup> Je, umewahi kuonja *Hii*? *Hii* ni nzuri, pia. Kasema, “Onjeni muone, Bwana ni mwema. Ina ladha ya asali mwambani.” Mara nyingi nimetoa tamshi hili, mara nyingi. Kwamba, wakati Daudi wa kale, aliyenena hayo katika Zaburi yake, aliposema, “Ina ladha ya asali mwambani.”

<sup>119</sup> Daudi, akiwa mchungaji, alikuwa na mkoba mdogo, waliubeba ubavuni mwao, nao sikuzote walibeba asali humo. Wachungaji wa kale hufanya hivyo, bado, huko—huko Palestina. Na wakati kondoo wao—wao wagonjwa wanaendelea, basi, muda si muda mwajua, alinyoosha mkono na anaenda kuchukua kipande kidogo cha hii asali, naye anaichukua na kuisugulia mwambani, jiwe la chokaa. Nao kondoo wanaipenda asali hiyo, kwa hiyo anaanza kuramba hiyo asali kutoka mwambani. Na kuna kitu fulani kuhusu chokaa ambacho huwaponya kondoo wagonjwa.

<sup>120</sup> Nami nawaambia, tuna mfuko mzima uliojaa asali hapa usiku wa leo, nasi tutaiweka juu ya Mwamba, Kristo Yesu. Nao kondoo wagonjwa wakianza kuramba, hakika utapata afya. Hiyo ni kweli, ramba tu, ramba, ramba. Na wakati ukiramba asali, mbona, kwa kweli utapata baadhi ya chokaa. Hiyo ni hakika kama kitu chochote kile. Sasa, hatutaiweka juu ya kanisa. Tutaiweka juu ya Kristo, ambapo ndipo mahali pake. Hiyo ni kweli. Maana, uponyaji ni wa Kristo, amina, kama baraka zingine zote za ukombozi. Angalieni.

<sup>121</sup> Na jambo lingine. Wakati hiyo ilipoanza kuanguka, Haruni aliamriwa atoke nje na kuokota pishi kadhaa zake.

<sup>122</sup> Sasa, kama wangejaribu kubakiza baadhi yake hata siku ya pili, iliharibika. Na hiyo sana sana iko miongoni mwa watu wa Roho Mtakatifu usiku wa leo. Mnajaribu kuwazia, “Vema, miaka ishirini iliyopita, tulikuwa na ujumbe mzuri. Tulikuwa na—tulikuwa na wakati mzuri.” Mna nini usiku wa leo? Hicho ndicho. Wao. . .

<sup>123</sup> Ilianguka kila usiku. Haikukosa hata wakati mmoja, ila tu kwenye—kwenye Sabato. Hiyo ni kweli. Na sasa Mungu ameishusha, mpya, kila usiku; kila siku, kila saa, inakuja.

<sup>124</sup> Angalia, hizo pishi zilihifadhiwa. Akasema, “Sasa, tazama, mtakapoingia nchini, nao watoto wenu waanze kuulizia jambo hili. . .” Kasema, “Kila kuhani sasa ambaye anangia katika ukuhani, akiisha kupata kibali cha kuja mahali Patakatifu, na kadhalika, na kutawazwa, kuhani, basi alikuwa na haki ya kuingia na kula fundi la mana asili iliyoanguka hapo mwanzo.” Ya kwanza kabisa iliyoanguka, waliokota na kuiweka katika pishi, na kuiweka, nayo ilihifadhiwa tu kwa ajili ya ukuhani.

<sup>125</sup> Sasa unasema, “Ndugu Branham, hiyo ina mfano gani siku hizi?”

<sup>126</sup> Mbona, sisi ni ukuhani. “Ninyi ni ukuhani wa kifalme, taifa takatifu, watu wateule, mkimtolea Mungu dhabihu za kiroho, matunda ya midomo yenu mkilishukuru Jina Lake.” Amina. Hiyo hapo. Sasa, basi, kwenye Siku ya Pentekoste, wakati Roho Mtakatifu alipokuwa akishuka; mana yetu.

<sup>127</sup> Sasa, kila kuhani huko nyuma, chini ya Agano la Kale, walipoingia kuwa kuhani, walijua wangepata fundi la ile mana

ya asili; si ya kujiokoa, ya kujitengenezea inayofanana nayo. Lakini wangepata baadhi ya ile ya asili.

<sup>128</sup> Vema, katika Siku ya Pentekoste, mana yetu ilipoanza kuanguka, Roho Mtakatifu alikuja kama upepo wa nguvu ukienda kasi. Hili hapa kundi la maskini watu wadogo, waungwana, mia moja na ishirini, katika chumba cha juu; milango imefungwa, madirisha yameshushwa, wameketi hapo nyuma, wakingojea ile ahadi. Naam, walikuwa pamoja na Yesu, hakika. Walijua nguvu Zake, na yote hayo, bali walikuwa wakiingojea ile ahadi.

<sup>129</sup> Hivyo ndivyo tunavyotaka usiku wa leo. Kuwa... Kama kundi hili la watu lingeweza kupatana kwa nia moja, kama walivyokuwa usiku ule, jambo lile lile lingejirudia usiku wa leo, papa hapa katika jengo hili, katika Louisville, Kentucky, ambalo lilijirudia kwenye Siku ya Pentekoste. Hiyo ni kweli. Loo, bila shaka, wangukuwa na wakosoaji wa aina ile ile hapa Louisville waliokuwa nao kule. Lakini, wote walikuwa mahali pamoja, kwa nia moja. Na ghafla...

<sup>130</sup> Akaja mhudumu, naye alikuwa na barua, nao wakaandika majina yao na kupeana mkono wa kuume wa ushirika, na kuingia katika ushirika wa kanisa? Hiyo huenda ikatukia leo, lakini haikuwa hivyo wakati huo. Hivyo ndivyo Waprotestanti wanavyolifanya. Mkatoliki anaenda madhabuhuni na kula ushirika wake wa kwanza; anatoa ulimi wake, anakula mkate mwembamba; naye kasisi anakunywa divai. Basi anakuwa hivyo.

<sup>131</sup> Lakini, ndugu, "Siku ya Pentekoste, walikuwa na nia moja, mahali pamoja, ndipo ghafla ukaja uvumi kutoka Mbinguni," mwanadamu hakuwa na uhusiano wowote nao, "kama upepo wa nguvu ukienda kasi. Ukaijaza nyumba yote waliyokuwa wamekaa." Nguvu za Mungu zikawapiga! Nao wakaingia barabarani, wakifanya kama kundi la wendawazimu; kama walivyofanya kule walipopitia Bahari ya Shamu. Hiyo ni kweli? Wakapiga mayowe. Wakaendelea. Wakayumbayumba. Wakagugumiza kwa midomo yao.

<sup>132</sup> Wao, loo, makelele mengi sana, wewe... mpaka hao watu, kanisa lenye heshima, likasimama nyuma na kusema, "Watu hawa wamelewa divai mpya.

<sup>133</sup> Haleluya! Mtaniita "mtakatifu anayejibingirisha," kwa vyovyote vile, kwa hivyo afadhali muanze sasa. Vema.

<sup>134</sup> Tazama, walikuwa wamejaa Divai mpya, hiyo ni kweli, ile Divai iliyotoka kwa Mungu, kutoka Mbinguni. Uliwahi kuona mtu mlevi? Anapenda tu kila mtu, unaona. Yeye hajali. Hivyo ndivyo mtu anavyokuwa wakati amelewa kwa Roho. Biblia ilisema, "Msilewe kwa vileo, kupita kiasi, bali mlewe kwa Roho." Roho wa Mungu anakufanya ulewe sana, hata unawasahau adui zako wote, na kila kitu. Kila mtu anakupenda. Yeye hajali ni nani

amesimama karibu nawe. Wewe ndiwe mtu mkubwa kuliko wote nchini wakati uo huo.

<sup>135</sup> Sijali kama jirani yako, anayeketi karibu nawe, alienda kwenye kanisa fulani la kiungwana; acha tu Roho Mtakatifu akushukie wakati mmoja, uone kinachotukia. Lewa vizuri kweli, kabisa kiasili, utaona kitakachotukia. Utasema, “Dada, nimeipata! Unaitaka, pia!” Hiyo ni kweli. Naam, bwana, jambo fulani litatendeka.

<sup>136</sup> Hao hapo, wote wamelewa kwa Divai mpya. Basi, sikilizeni, baadhi yenu akina dada hapa, je, mlijua kwamba bikira Mariamu mbarikiwa alikuwa humo? Sasa, ilimbidi kwenda kule. Ilimbidi mama yake Yesu Kristo aende kule na kujumuishwa katika kundi hilo la watu, amelewa sana kwa Roho hata akayumbayumba kana kwamba alikuwa amelewa wiski ama chochote kile.

<sup>137</sup> Nawe unafikiri utaenda Mbinguni kwa kupenya kisiri kanisani na kuweka kitabu chako cha nyimbo chini ya mkono wako, na kwenda kule kila Jumapili asubuhi, na kengele inalia, na kuketi na kusikiliza baadhi ya...na kurudi? Kamwe hutaenda.

<sup>138</sup> Itakubidi uje kwa njia hiyo, maana hiyo ndiyo njia pekee ambayo Mungu amewahi kuiweka, na amepata kuiweka. Nawe utaitembelea, la sivyo hutakuwepo Huko. Mimi si hakimu wako, lakini ninahubiri Injili. Hiyo ni Kweli kabisa. Yule bikira aliyebarikiwa alikuwa pale pale, alitenda kijinga kama hao wengine walivyofanya, amelewa tu kama hao wengine. Hawa wanaume na wanawake, kila mmoja wao, alikuwa amejaa Divai mpya. Kama Mungu aliwahi kubadilisha mpango huo, niwekee kidole chako kwenye hilo Andiko; halipo. Hapana, bwana. Ilikuwa ni moja kwa moja hadi mwisho wa wakati, hivyo, moja kwa moja mpaka mwisho wa Biblia, na litakuwa ni jambo lile lile Yesu atakapokuja.

<sup>139</sup> Tazama! Walipokuwa wamelewa Divai hiyo mpya, tazama, tuone kama Mungu aliweka pishi kwa ajili yenu nyote. Vema.

<sup>140</sup> Hawa hapa wote walikuwa wamesimama pale nje, na maskini mhubiri mwoga mzee jina lake Petro, yule “mwamba mdogo,” alihofia sana mahali pake hata akamkana Yesu, kisha akakimbia na kuomba kabisa, na ilimbidi kukusanyika pamoja nao. Alisimama juu ya sanduku la sabuni au chochote kile, akasema, “Mbona, ninyi watu wa Uyahudi, na ninyi mnaokaa Yerusalemu!” Hao walikuwa madaktari, ma D.D. Loo, akasema, “Ninyi wanaume ambao...na watu wa Israeli, na wakaaji wa Yerusalemu, na kadhalika, hili na lijulikane kwenu. Hawa hawajalewa, kama mnavyodhani, kwa kuwa ni saa tatu ya mchana. Lakini hili ni lile...”

<sup>141</sup> Kama hili si Lile, ninataka kuweka hili mpaka Lile litakapokuja. Hilo ni jambo moja.

<sup>142</sup> Akasema, “Hili ni lile lililonenwa na nabii Yoeli, ‘Itakuwa katika siku za mwisho, asema Mungu, nitamwaga Roho Yangu juu ya wote wenye mwili; wana wenu na binti zenu watatabiri; na juu ya wajakazi wangu na watumishi Wangu wanawake nitaimwaga Roho Yangu, nao watatabiri; nami nitaonyesha ishara juu mbinguni, na duniani; na nguzo za moto, na moshi, na mvuke; na itakuwa, kabla haijaja ile siku ya Bwana iliyo kuu na ya kuogofya, kila atakayeliitia Jina la Bwana ataokoka.’”

<sup>143</sup> Kundi hilo la makuhani wa mtindo wao wenyewe, wenye mavazi marefu, wanafiki, lilisema, “Je, tutendeje tupate kuokolewa?”

<sup>144</sup> Petro akasema, “Tubuni, kila mmoja wenu, mkabatizwe katika Jina la Yesu Kristo kwa ondoleo la dhambi zenu, nanyi mtapokea kipawa cha Roho Mtakatifu.” Ni ya muda gani? “Kwa maana ahadi hii ni kwa ajili yenu, na kwa watoto wenu, na kwa wale walio mbali, na kwa wote watakaotwa na Bwana Mungu wetu wamjie.”

<sup>145</sup> Basi, kila mtu anayetubu na kubatizwa katika Jina la Yesu Kristo, kisha Mungu anampa ubatizo wa Roho Mtakatifu, hapati kitu kinachofanana na ile mana ya asili, lakini, yeye hapati tu funda la mana ya kwanza, bali anapata moyo mzima uliojaa Roho Mtakatifu yeye yule.

<sup>146</sup> Huenda ukasema, “Ipunguze hiyo kidogo.” Najua nina sauti kubwa kidogo juu ya hilo, lakini siwezi kujizuia. Angalieni, tazameni. Siwapigii kelele. Ninaweza kuwa narudisha mwangwi kwake. Lakini, loo, kama ungejisikia kama nilivyojisikia, ungepaza sauti, pia.

<sup>147</sup> Angalieni, loo, moyo mzima uliojaa ile mana iliyoshuka hapo mwanzo; Roho Mtakatifu yule yule aliyeshuka wakati huo, anashuka sasa. Naye angeenda wapi? “Kwenu, kwa watoto wenu, wale walio mbali,” Louisville, Kentucky, “na wote watakaotwa na Bwana Mungu wetu wamjie, watapokea kitu kile kile tulicho nacho hapa.”

<sup>148</sup> Hivyo ndivyo Yeye alivyosema. Mungu alilibariki. Yeye akalihubiri. Roho Mtakatifu akalileta; nimelipata; hilo latosha. Amina. Hilo, hilo ni zuri tu kutosha kwangu. Nililiamini Neno Lake; Yeye akafanya hivyo. Ukilitaka, unaweza kulipata, pia. Hiyo ni kweli.

<sup>149</sup> Basi ondoka kwenye ha—hali ya kufa, na uamke, na ujitikise tu namna hiyo na uamke. Basi jambo la kwanza, angalia pande zote na kila kitu kitaonekana tofauti kwako. Yule jamaa ambaye usingeweza kuzungumza naye, utaharakisha kwenda kwake na kuzungumza naye; naam, bwana, inabidi tu kuzungumza naye, ni hivyo tu. Loo, mambo hayo yote, unarudisha zana hizo kuukuu za matairi, na ninii zote...vitu hivyo vyote ulivyotoa hotelini wakati huo. Hiyo taulo kuukuu uliyokifunikia kile chombo cha fedha ulichochukua mezani; utaharakisha, upate kuirudisha.

Hakika utairudisha. Naam, bwana. Itakufanya kiumbe kipya katika Kristo Yesu. Sasa mtazame Mariamu. Loo, jamani!

Inabidi tuharakishe. Tunaendelea sawasawa.

<sup>150</sup> Hawa hapa wanaenda, wakipitia nyikani sasa, baada ya ule mkutano wa mtindo wa kale. Sasa wako safarini mwao. Je, si ajabu kwamba waliongozwa moja kwa moja hadi kwenye Bara ya Sini, moja kwa moja hadi nyikani, moja kwa moja hadi kwenye che—chemchemi ya maji machungu? Unaweza kuwazia Mungu akiwapeleka watoto Wake, mara baada ya wao kuokoka na kujazwa na Roho Mtakatifu, kwenye chemchemi za maji machungu? Hakika. Angependa kueleza upendo Wake kwao tena. Hiyo ni kweli. Wakafika kule juu.

<sup>151</sup> Unajua, unapompata Roho Mtakatifu, unakabiliana na vikwazo vingi. “Mateso ya mwenye haki ni mengi, lakini Mungu humponya nayo yote.” Mungu hukuleta juu moja kwa moja, ukikabiliana nayo, ili aweze kukuonyesha uweza Wake na wema Wake.

<sup>152</sup> Kama vile nilivyosikia hadithi ya mchungaji huko Yerusalemu, ambaye alikuwa amevunja mguu wa kondoo wake. Wakasema, “Mbona, wewe mchungaji katili. Kwa nini ukavunja mguu wa kondoo?”

<sup>153</sup> Kasema, “Vema, hakufanya kama ananipenda. Kwa hivyo nilifikiria ningemvunja tu mguu, kusudi inibidi nimpe uangalizi maalum, ndipo basi atanipenda tangu hapo na kuendelea.”

<sup>154</sup> Wakati mwingine inambidi Mungu kukulaza kichalichali, kwa maradhi, hata daktari anasema utakufa. Mungu anaweza kukupa uangalizi maalum kidogo ili umpende zaidi. Hiyo ni kweli.

Wengine kupitia majini, wengine kupitia mafuriko,

Wengine kupitia majaribu mazito, lakini wote kupitia kwa Damu;

Yesu analiongoza Kanisa Lake.

<sup>155</sup> Sasa, walipokuwa pale, nayo maji yalikuwa machungu wala wasingeweza kuyanywa, Mungu alifanya njia. Maskini mti wa kale ukiyumbayumba pale ukingoni, Musa aliukata tu na kuutupa majini, ulikibadilisha kitu hicho chote; maji mazuri, matamu.

<sup>156</sup> Sasa unapokuja dhidi ya mojawapo ya maji yako machungu, ama kitu kingine kama hicho, kuna mti, usiku wa leo, tukizungumza kiroho, unaoning’inia juu ya Golgotha, ama ulimwengu, usiku wa leo, ambao utayafanya matamu maji yoyote machungu ambayo huenda yanakuongoza. Hiyo ni kweli. Kalvari itafanya kila ujuzi kuwa mtamu. Mara nyingi tunaingia kwenye maeneo magumu, nasi tunashangaa ni vipi. Kwa hiyo nafunga macho yangu wakati mwingine, na kuwazia, “Huko

Golgotha, ambapo Mkombozi wangu alimwaga damu na kufa kwa ajili ya maisha yangu,” ndipo majaribu yangu yalionekana kuwa madogo sana. Ninayatupa tu kando na kuendelea. Inalifanya tamu. Inatia utamu kila ujuzi niliowahi kupata. Yeye sikuzote huutia utamu, ninapofika kwenye maji yangu ya Mara.

<sup>157</sup> Sasa, tunakaribia kuwashika sasa huku nyikani, baada ya hizo ishara zote kuu na maajabu. Uamsho ulikuwa umetulia. Ndipo muda si muda mnajua, wakati uamsho ulipotulia, mbona, walisahau yote kuhusu miujiza.

<sup>158</sup> Je, hiyo si ni kama watu siku hizi? Wanasahau yale Mungu aliyofanya mwaka jana. Yale Mungu aliyofanya hapa kwenye mkutano katika shule ya upili, mnasahau yote kuyahusu. Mnaona? Aliyofanya Mungu, tunayasahau tu.

<sup>159</sup> Sasa, angalieni, na kwa sababu wanaanza kubishana wao kwa wao, “Vema, mimi kwa kweli, hata hivyo, mimi ni Mmethodisti. Kanisa letu ndilo kubwa kuliko yote.” “Mimi ni Mbaptisti, nami nitawaambia sasa hivi, tunaamini katika usalama wa Milele, nasi tunao. Ninyi nyote hamna fundisho, hata hivyo.” Hapo ndipo unapoingia katika shida, na ruzuku yako ya maji inakatizwa. Hiyo ni kweli. Hiyo ni kweli.

<sup>160</sup> Hapo ndipo, jangwani, anapoishi jangwani, anaanza kunung’unika, kunung’unika na kulalamika. “Naam, nitakwambia. Nitakwambia, wakati yule mchungaji mzee alipokuwa hapa, yule mhubiri mzee aliyehubiri dini hiyo ya mtindo wa kale namna hiyo, si—sijui kama alikuwa sahihi au la. Nitakwambia, a—alimkasirisha sana mama yangu, usiku mmoja, akaenda nyumbani. Nami nitakwambia, alivurugika sana, kitu kama hicho.” Alipaswa kuvurugika. Hiyo ni kweli. “Loo, sijui kama ninataka kusikia zaidi ya Hilo, ama la.” Basi hapo ndipo ruzuku yako ya maji inapokatika. Hiyo ni kweli. Hapo ndipo unapoingia jangwani.

<sup>161</sup> Wakaanza kunung’unika. Wakasema, “Roho ze—zetu zinachukia mkate huu mwepesi.” Baada ya kuacha vitunguu saumu na vitunguu vya Misri, nao walikuwa wakila chakula cha Malaika, na wangali wanalalamika. Je, hilo si ni kama kanisa? Sasa ninashuka kuja kwa watu wa utakatifu sasa, ninyi nyote; naam, ninyi nyote. Wakila chakula cha Malaika, kisha wakasema, “Laiti tungalikuwa tumerudi Misri, kula vitunguu saumu zaidi.”

<sup>162</sup> “Clayton McMichen na Wildcats wake watakuwepo kwenye baa usiku wa leo. Kama singekuwa nimejiunga na maskini kanisa hilo, ningalishuka niende kule.” Hata afadhali uende. Ilipo hazina yako, ndipo ulipo moyo wako pia. Hukupata chochote kamwe wakati ulipoanza. Hiyo ni kweli. Hiyo ni kweli. “Loo, ningependa kufanya *hivi*, ama kufanya *vile*.” Wewe hapo, malalamiko kila wakati.

<sup>163</sup> Nao wakayaacha maji ya Misri yaliyojaa matope, wapate kunywa maji safi kutoka katika Mwamba wa Miaka, nao walikuwa wakinung'unika juu Yake. Wakaondoka mahali pale walipokuwa wale waganga wakuu wa Misri waliojigamba, wenye majivuno makubwa na kadhalika, wapate kuwa pamoja na Tabibu Mkuu. Wakaondoka mahali waliposema, kwamba, "Siku za miujiza zimepita," wapate kuwa pamoja na watu waliokuwa na ishara na maajabu yakiwafuata, na wangali wakilalamika. Loo, jamani! Naam, bwana. Huko chini, bila shaka, Wamisri, walikuwa Wamataifa baridi, wasiojali. Hawakuamini katika kitu kama miujiza.

<sup>164</sup> Halafu, walikuwa hapa nje ambapo walikuwa na Nguzo ya Moto iliyowazunguka. Tunayo usiku wa leo. Walikuwa huko nje ambako walikuwa na furaha kambini, wakipaza sauti, miujiza ikitendeka, na kila kitu, na kisha kulalamika juu yake. Hiyo ndiyo sababu yale maji yalikauka, hiyo ndiyo sababu hawakuwa na kitu cha kula wala kunywa, kwa sababu walikuwa wakinung'unika.

<sup>165</sup> Na hiyo ndiyo shida ya makanisa yanayozunguka Louisville, usiku wa leo; kunung'unika, kulalamika. Rehema! Rudini kazini. Ndivyo hivyo.

<sup>166</sup> "Basi jamaa huyu ni nani, Musa? Kwa nini tulisikiliza, kumsikiliza mhubiri huyu mtakatifu anayejibingirisha, kwa vyovyote vile? Tunafanya nini huku nje?" Ndipo ruzuku yao ya maji ikakauka.

<sup>167</sup> Ninawaza juu ya Musa, yule mtu mashuhuri. Alifundishwa katika he—hekima yote ya Wamisri. Hebu tumtazame kwa dakika chache tu. Hebu tumchukue Musa, kwa dakika moja tu. Mwangalieni jamaa huyo. Alikuwa. . .

<sup>168</sup> Wamisri, walitushinda kwa mbali siku hizi, inapofikia kwenye sayansi yetu ya kitabibu. Walitushinda kwa mbali sana. Mambo mengi wangeweza kufanya ambayo sisi tusingeweza.

<sup>169</sup> Naye Musa alikuwa na dawa zote. Na alipokuwa huko nje, wazia, Musa alikuwa na kama watu milioni mbili pamoja naye. Alikuwa na watoto wadogo. Alikuwa na wazee, wanawake wakongwe. Alikuwa na vilema, na vipofu. Watoto walizaliwa, maelfu yao, katika muda wa juma moja. Naye Musa, Dk. Musa, alikuwa huko nje nyikani pamoja na watu hawa wote. Ningependa kuangalia ndani ya sanduku lake la dawa, nanyi je? Ningependa kuona kile ambacho Dk. Musa alikuwa nacho kwenye sanduku lake la dawa. Hebu tuchungulie tu kidogo kwenye sanduku lake la dawa tuone kile alichokuwa nacho.

<sup>170</sup> "Musa, mbona, kwani una nini hapo ndani, Musa?" Mbona, tunaona ya kwamba kwenye safari hiyo yote ya miaka arobaini, zaidi ya watoto milioni mbili zaidi walizaliwa. Hiyo ni kweli. "Kwani ulitumia nini, Musa? Ulitumia nini kwa uchungu huo wote na maumivu na kansa, na upofu, na uziwi, na

ububu? Mbona, wananiambia, ya kwamba ulipotoka nyikani, hapakuwapo na mnyonge miongoni mwao.” Aisee, je, baadhi ya madaktari hawa si wangependa kuangalia ndani ya hilo, hilo kabati la dawa?

<sup>171</sup> “Na jambo lingine, Musa, uliwanyunyizia nini watu hao, hata nguo zao hazikuchakaa? Viatu vyao havikuchakaa, wakitembea juu ya mawe hayo.” Ikiwa umewahi kuwa huko, unajua jinsi hilo jangwa linavyoonekana, wanaichakaza jozi ya viatu katika siku tatu. Nao hata hawakuchakaza chembe moja ya ngozi kutoka kwavyo, katika miaka arobaini. “Musa, nini kilichokuwa kwenye kabati lako la dawa?”

<sup>172</sup> Hebu tuangalie ndani yake. Ninamwona, “Nina agizo moja, ‘Mimi ndimi Bwana nikuponyaye.’” Hilo latosha. Amina.

<sup>173</sup> Kasema, “Loo, Musa, baba yangu amekuwa hapa, ameanguka hivi punde na kuvunjika mguu. Utampa nini?”

<sup>174</sup> “Ngoja niangalie nione. ‘Mkiitii sauti Yangu, mfanye yote niwaamuruyo, sitatia yoyote ya magonjwa haya juu yenu, kama Wamisri, kwa kuwa Mimi ndimi Bwana nikuponyaye.’ Mwambie hivyo.” Akapata afya. Amina. Hiyo ni kweli.

“Loo, yeye ni mahututi! Mtoto wangu ana mchango, au nimonia, mbaya sana! Dk. Musa, nifanyeje?”

<sup>175</sup> “Hebu nione nilicho nacho. ‘Mimi ndimi Bwana nikuponyaye.’” Hiyo inatosha. Amina. Wakaenda zao. Hiyo ni kweli. Wakiendelea, wakishangilia. Hilo ndilo lote alilohitaji, “Mimi ndimi Bwana nikuponyaye.”

<sup>176</sup> Kati ya ahadi mia sita na kitu, ahadi dhahiri za uponyaji wa Kiungu, katika Agano Jipya pekee, na hata hivyo tunampigia Mungu swali, usiku wa leo. Je, ile Hukumu itamaanisha nini kwetu? Kweli.

<sup>177</sup> “Mimi ndimi Bwana nikuponyaye.” Naam, bwana. Hilo ndilo alilokuwa nalo, Musa, Dk. Musa alikuwa nalo katika nyanja yake, katika ninii yake. . . kwenye kabati lake la dawa, ilikuwa hivi, “Mimi ndimi Bwana nikuponyaye.” Kwa hiyo aliponya magonjwa yote, na kuwaweka kikamilifu, naye akawaleta moja kwa moja kupitia nyikani, hadi kwenye nchi ya ahadi. Loo, jamani!

<sup>178</sup> Waliachana na wale waganga wote wakubwa, wenye kiburi, wapate kuwa pamoja na Tabibu huyu Mkuu. Walikuwa wameachana na kundi hilo la watu waliokuwa baridi, wa kawaida, na wasiojali, wakisema, “Hakukuwa na kitu kama miujiza.” Na papa hapa, Nguzo ya Moto ilikuwa inaning’inia juu yao. Watu walikuwa wanaponywa. Kila kitu, na chochote walichohitaji kiliwasilishwa mara moja kwao, na bado walikuwa wakilalamika walipotoka majini. Lakini basi katika neema kuu ya Mungu, katika hayo yote. . .

179 Kama vile mlivyo hapa Louisville usiku wa leo, katikati ya kilio hiki chote, “Siku za miujiza zimepita. Shirika la Matibabu linajaribu kukomesha uponyaji wa Kiungu, kote nchini.” Kamwe hamtaweza kuukomesha. Afadhali muachane nao sasa. Hamwezi kuusimamisha zaidi ya vile mnavyoweza kulisimamisha jua. Hiyo ni kweli.

180 Hapa miaka michache iliyopita, nilipoanza huku Jeffersonville kwa mara ya kwanza, nilikuwa nikihubiri uponyaji wa Kiungu. Haukuwa umejulikana, takriban, kwa miaka. Lilikuwa jambo gumu. Lakini, ndugu, usiku wa leo kuna mamilioni yao, kila mahali, wakipaza sauti. Ati ujaribu kuuzuia? Huwezi. “Mimi Bwana, nimeipanda; nitaimwagia maji, mchana na usiku, asije mtu akaitoa mkononi Mwangu.”

181 Hapa si muda mrefu uliopita, nilikuwa nikiwatazama shorewanda wadogo kwenye Sanamu ya Uhuru. Walikuwa wamelala tu pale. Jamaa hao wadogo walikuwa wamelala pande zote, chini ya mwangaza. Nami nikasema, “Je, hilo limesababishwa na nini?” kwa kiongozi.

182 Akasema, “Walipasua bongo zao, jana usiku, katika ile dhoruba. Waliingia kwenye taa, nazo hizi taa zingewapeleka kwenye usalama, lakini walikuwa wakijaribu kuzima hizi taa. Nao wakapasua bongo zao, wakijaribu kuzima taa.”

183 Nikasema, “Utukufu kwa Mungu!” Nadhani alifikiria nilikuwa wazimu. Nikasema, “Hilo linanikumbusha baadhi ya watu hawa wanaojaribu kuupiga uponyaji wa Kiungu na Nguvu za ufufuo wa Yesu Kristo.” Utaupasua ubongo wako; hutaweza. Ukubali tu, na uruke uende mahali pa salama, ndani yake. Hiyo ni kweli. Amina.

184 “Nena na mwamba, Musa,” Mungu alimwambia Musa, “nao utatoa maji yake, kutoa maji Yake.”

185 Hapa si muda mrefu uliopita, nilikuwa nikitazama picha fulani katika jumba fulani la makumbusho, ya kupigwa kwa mwamba huu. Na ilionekana kama kijito kidogo cha maji kikimwaga maji, yapata ukubwa wa sindano ya kushona. Nikawazia, “Jinsi wasanii hawa wanavyoweza kuwa wa kimzaha!” Mbona, ndugu, ningeweza kunywa kitu hicho nikimalize kama ningekuwa na kiu sana. Naam, bwana.

186 Je, mnajua wale Musa aliopaswa kuwanywesha kutoka kwenye huo Mwamba? Alikuwa na watu zaidi ya milioni mbili, mbali na wanyama wote. Ilihitaji kama galoni elfu arobaini kwa dakika moja, ku—kuwanywesha, hao. Haleluya!

187 Hilo linanikumbusha mtu fulani katika dini yao. Una dini ya kutosha tu kwenda kwenye shule ya Jumapili Jumapili asubuhi, kukunyunyizia kidogo tu na kukulowesha kidogo.

188 Ninapenda kuketi kwenye Chemchemi ambapo vibubujiko hutoka, haleluya, vya kutosha kunipitisha katika Umilele.

Haleluya! Ninafurahi kwamba nilihama kutoka mahali hapo penye unyevu; hadi kwenye kijito ambapo kinabubujika tu wakati wote. Naam, bwana.

<sup>189</sup> Watu wana dini ya kutosha tu kuwafanya wenye mashaka. “Vema, siwezi kuketi zaidi ya dakika kumi. Jamani, salaala, mhubiri huyo ana maneno mengi ya kuchosha?” Wokovu wako una kina kipi? Hiyo ni kweli.

<sup>190</sup> Unapanda kwenda Jumapili asubuhi na kusema, “Vema, nitapanda huko nikasikie wanachosema.” Ndipo unapata ugomvi mmoja mdogo na kurudi, na hayo ni karibu yote uliyo nayo.

<sup>191</sup> Ndugu, nitakwambia, Musa alipoupiga huo Mwamba, ulimwagilia maji nyika nzima. Amina. Naam, bwana. Kitu pekee, kila kitu walichohitaji, walianguka tu chini wakanywa, wakanywa, wakanywa hadi wakashiba kabisa. Bado, maji zaidi yalikuwa yanakuja, yapata galoni elfu arobaini kwa dakika. Liwazie, ni watu wangapi, watu milioni moja, watu milioni mbili wangeweza kunywa, katika muda wa dakika moja; watu wenye kiu, mbali na ngamia, na wanyama, na vitu walivyokuwa navyo. Nayo Biblia ilisema, “Yalifoka kwa wingi.” Yalibubujika tu, kupitia nyikani.

Hivyo ndivyo Yesu Kristo alivyotoa Roho Mtakatifu.

<sup>192</sup> Sio kidogo tu kusema, “Vema, ninaamini nitaenda na kujiunga na kanisa.” Loo, jamani! “Loo, siwezi kustahimili kelele hizo. Hizo zinanipa mitetemeko.” Ukipata kufa, ungeganda hadi kufa kama ungefika Mbinguni, maana, ndugu, utasikia kelele utakapofika Huko. Biblia ilisema wanapaza sauti “haleluya,” mchana na usiku; mchana kutwa, kwa sababu hakuna usiku. Hiyo ni kweli. Hakika utakufa utakapofika Mbinguni, siku ya pili Kule juu. Naam, bwana. Naam, wewe ulininii tu. . . ulichofanya, ulienda tu ukalowa maji, kidogo.

<sup>193</sup> Je, mbona usiketi karibu na hilo bubujiko, uliache libubujike mpaka likuoshe uwe. . . haleluya, katikati, na mpaka ujipoteze na usijue mahali ulipo. [Sehemu tupu kwenye kanda—Mh.] Hivyo ndivyo unavyotaka kufikia.

<sup>194</sup> Nilishikilia kumwambia mjomba wangu, baba yangu, “Jamani, naweza kuogelea,” katika kidimbwi hiki kidogo hapa juu Utica Pike.

<sup>195</sup> Siku moja, baba alirudi na kuketi kwenye kalvati, akasema, “Nataka kukuona ukiogelea.” Maskini kidimbwi hicho kilikuwa na kina karibu *hivi*. Nilikuwa nimesimama juu ya kijisanduku cha sabuni. Nikavua vitu vyangu, na kushika pua yangu namna *hii*, na kuruka juu-chini kwenye hicho kijisanduku cha sabuni. Nilipiga, matope yakaruka pande zote mbili, na nikaanza kurashia matope.

Nikasema, “Ninaendeleaje, Baba?”

<sup>196</sup> Kasema, “Ondoka hapo.” Ati kuogelea? Huku nikitambaa matopeni, wakati wote.

<sup>197</sup> Tuna washiriki wengi wa kanisa wanaotambaa matopeni, pia. Hiyo ni kweli. Hiyo ni kweli, watambaa matopeni. Naam, bwana.

<sup>198</sup> Siku moja, mjomba wangu alinipeleka kwenye mashua nami nilikuwa nikijivunia kuogelea; hapa katika Mto Ohio, yapata futi ishirini za maji. Alichukua tu kasia na kunigonga nikaanguka majini, akasema, “Sasa vipi kuhusu hilo?” Amina. Haleluya! Ilinibidi kuogelea la sivyo nizame, basi. Loo, jamani!

<sup>199</sup> Afadhali nilizoe sasa. Uende kwenye bubujiko, ambapo Mungu hufungua mwamba kule nyikani na kuyabubujisha tu. “Sema na Mwamba,” Akasema, “nao utatoa maji Yake.”

<sup>200</sup> Labda, rafiki yangu, usiku wa leo, labda unaangamia. Unapaswa kunena na Mwamba. Hiyo ni kweli.

<sup>201</sup> Labda umeenda kila mahali. Labda umeenda kanisani, na kujiunga na Methodisti, na kujiunga na Baptisti; nao wakakukasirikia sana, kisha ukaiendea Presbiteri; halafu ukarudi kwa Wapentekoste, kule kwa Nazarayo, ukashuka kwa Pilgrim Holiness. Nawe ungali huelewi.

<sup>202</sup> Nena tu na Mwamba, usiku wa leo. Ninii tu... Je, wewe uko katika nafasi ya kuemezana Naye? Naam. Alisema, “Nena na Mwamba, Naye atatoa maji Yake.” Atatoa maji Yake, kama ukininii tu... Si lazima umpige, tena. Nena Naye tu. Kwa hali ya kirafiki tu, nena Naye.

<sup>203</sup> Labda umekuwa kwa daktari. Labda umefanya kila kitu ambacho unajua jinsi ya kufanya, kujaribu kupata afya. Labda umefanya tu kila kitu kilicho katika umezo wako, karibu, wala huwezi kupata afya. Kila daktari, umepitia kila ofisi unayojua kupitia, naye daktari akasema, “Wewe... Hakuna kinachoweza kufanywa kwa ajili yako.” Kwa nini usiunene Mwamba, usiku wa leo? Ataninii... Ana maji ya Uzima pale kwa ajili yako, yakikupa Uzima kwa wingi zaidi.

<sup>204</sup> Wakati mmoja kulikuwako na mwanamke, katika Biblia, jina lake Hajiri. Ninamwazia. Nami ninajiandaa kufunga; muda. Kulikuwa na mwanamke, jina lake Hajiri, naye alikuwa na mtoto mdogo. Alifukuzwa akaenda nyikani, akiwa na chupa moja ndogo ya maji. Akakilisha kitoto hicho kidogo, siku nzima. Lakini maji yakaisha, mnamo yapata adhuhuri, basi mtoto huyo mchanga alikuwa akipiga mayowe na kulia. Midomo yake midogo ilikuwa imekauka na ulimi wake ulikuwa ukivimba. Maskini mama mpendwa, angefanyaje? Alikuwa ametafuta kila mahali alipoweza, apate maji, lakini hakuna maji yaliyopatikana. Hangeweza kuvumilia kuona mtoto huyo akifa; kwa hiyo akamweka chini ya kichaka, akaenda umbali wa kadiri ya mtupo wa mshale.

205 Ndipo akapiga magoti na kunena na Mwamba. Aliponena na Mwamba, Malaika alijibu na kusema, “Hajiri, ni kitu gani kile kinachobubujisha huko?”

206 Kulikuwa na kisima kizima, kilichojaa maji, ambacho bado kinabubujika hata wa leo. Baada ya karibu miaka elfu nne, bado kinabubujika leo hii. Chemchemi ambayo Hajiri. . . hapo, hiyo, kingali kinabubujika leo hii. Alinena na Mwamba, nao Mwamba ukatoa maji.

207 Kulikuwa na baadhi ya watoto wa Kiebrania walioingia kwenye tanuru ya moto, siku moja, nao wakanena na Mwamba. Naye Mwamba alikuwa pamoja nao.

208 Kulikuwa na mwanamke aliyetoka Samaria, wakati mmoja. Alikuwa amevunjika moyo. Alikuwa mwenye dhambi, na alikuwa na mambo mengi sana yakining’inia maishani mwake, labda. Naye alikuwa amevunjika moyo. Alienda kwenye kisima cha Yakobo ili kupata nafuu, naye angerudi. Angeenda kwenye kisima cha Yakobo, na kurudi. Basi siku moja aliuweka mtungi wa maji chini, naye alikuwa amesimama pale, amevunjika moyo. Ndipo hapo akasimama yule Mwamba, akisimama karibu naye. Akasema na Mwamba huyo. Akampa chemchemi kubwa nafsini mwake. Akakimbilia mjini. Hakuja kuchota, tena. Alikuwa na Uzima. Akasema, “Njoni, mwone Mtu aliyeniambia kila kitu nilichowahi kufanya. Haimkini huyu kuwa ndiye Kristo?” Alinena na Mwamba, nao Mwamba ukatoa maji Yake.

209 Kulikuwa na maskini mwanamke ambaye alikuwa amepoteza pesa zake zote kwa madaktari, mabingwatapeli, ambao walikuwa wamechukua pesa zake zote. Hawangeweza kukomesha huko kutokwa na damu. Pengine alikuwa ameweka shamba lake rehani, na labda akaliuza. Naye alikuwa ameketi, akifuma siku moja, naye akasikia Kitu fulani kikishuka barabarani. Akanena na Mwamba. Huyo Mwamba akageuka na kusema, “Ni nani aliyenigusa?” Ilikuwa imekwisha aliposema na Mwamba. Akampa bubujiko la Uzima, ambalo lilikomesha kutokwa na damu. Ilizima, upesi.

210 Kulikuwako na maskini ombaomba kipofu amesimama kando ya ukuta, siku moja, akitetemeka kwa baridi. Kila kitu alichokuwa nacho kilikuwa kimekwisha. Naye huyu hapa, na mwenye mashaka, na watu wakipita. Alisikia kitu Fulani kikija; kasema, “Ni kitu gani?” Akasema na Mwamba.

211 Ingawa, washiriki wa kanisa lake, waliomzunguka, walijaribu kumzuia, wakisema, “Hakuna haja. Huwezi kuupata. Kaa mbali. Tulia.”

212 Lakini alilia zaidi, “Ewe mwana wa Daudi, unirehemu! Nirehemu!” Naye akasema na Mwamba, naye Mwamba akampa bubujiko, ndipo macho yake yakafunguka.

213 Mwamba uo huo uliokuwa nyikani uko hapa leo. Huwafanya watu washangilie.

214 Siku moja, Yerusalemu nzima ilikuwa imesimama kumwona mponyaji wa Kiungu, mtakatifu anayejibingirisha, akiingia mjini; huku watu wachache wakiwa wamesimama pale, wakipiga mayowe kwa sauti zao zote, “Hosana! Hosana, kwake Yeye ajaye katika Jina la Bwana!”

215 Wale wanaojiita washiriki wa kanisa waliokuwa huko nje wamevaa majoho yao marefu, na D.D zao nyuma yao; wakasema, “Hebu wanyamaze. Jamani, wanafanya mizizimo ipitie mgongoni mwangu, na kadhalika. Wanyamazishe.”

216 Akasema, “Wakinyamaza, mawe yatalia mara moja.” Kwa nini hivyo? Mwamba ule ule uliokatwa mlimani, bila kazi ya mikono, ulikuwa unakuja, ukiviringika mpaka Yerusalemu. Mawe madogo yalikuwa yakiunywea. “Sema na mwamba, nao utatoa maji Yake.”

217 Kama unahitaji wokovu, usiku wa leo, sema na Mwamba. Utatoa maji Yake. Kama umerudi nyuma, usiku wa leo; sema na Mwamba, utatoa maji Yake. Kama uko hapa, usiku wa leo, na bila Kristo; umejaribu kila kanisa lililopo, mjini, kupata wokovu; sema na Mwamba, utatoa maji Yake. Unaamini? Ikiwa umerudi nyuma, ukamwacha Mungu, unafikiri hakuna nafasi kwako; nena tu na Mwamba, nao utatoa maji Yake.

218 Je, unaamini hilo, kwa moyo wako wote? Je, unaamini ya kwamba Mungu angelijalia? Kwa moyo wako wote, unaamini? Haleluya! Yuko hapa usiku wa leo.

219 Ikiwa wewe ni mgonjwa, na umejaribu kila kitu duniani. Umejaribu kuingia kwenye mstari wa maombi, wala huwezi kuingia kwenye mstari wa maombi. Umekuwa na kadi za maombi, na ukakataliwa. Umeenda kwenye mkutano mmoja; ukaenda kwenye mkutano mwingine. Umepakwa mafuta na mchungaji. Umepitia mstari huu wa maombi. Umekuwa kwingine kote, na huwezi kupona.

220 Kwa nini usinene na Mwamba sasa? Atatoa maji Yake. Hiyo ni kweli. Kwa nini usimjaribu mara moja? Anza kuzungumza Naye, sasa hivi, wakati akiwa jengoni. Uwepo Wake upo papa hapa sasa kuponya kila mmoja wenu. Ninaamini hilo. Ninajua hilo, kwa moyo wangu wote. Naamini. Na kuna mambo ambayo sijui, lakini kuna mambo niyajuayo. Nami ninajua kwamba Yesu Kristo, Mwana wa Mungu aliye hai, yuko papa hapa.

221 Wakati nikijaribu hata kufanya wito wa madhabahuni sasa hivi, moyoni mwangu, maono yanatokea kote jengoni sasa—sasa hivi. Loo, hiyo ni kweli. Nguvu za Mungu ziko papa hapa. Hiyo ni kweli. Nilimwona akitembea hapa. Imeanza kuniingiza kutoka upeo mmoja hadi mwingine, sasa hivi; maana kuna watu wagonjwa hapa, na maombi yenu ndiyo yanayosababisha jambo hilo; kulithibitisha Neno la Mungu, akisema Yeye yuko papa hapa apate kunenewa, usiku wa leo, Mwamba ule ule uliosimama na kuyatambua mawazo yao. Aliona mahali yule mwanamke

alipokuwa, aliyekuwa na shida ya kutokwa damu, na kadhalika. Yuko hapa sasa. Ikiwa utazungumza Naye, atatoa maji Yake. Mnaamini hilo kwa moyo wenu wote?

<sup>222</sup> Waonaje, mama? Pamoja na... Papo hapo katikati. Sasa, huna kadi ya maombi, sivyo? Huyu mama aliye na kitu cheupe shingoni mwake, aliyeketi papo hapo. Una kisukari, sivyo? Huna kadi ya maombi, sivyo? Huhitaji kadi yoyote ya maombi. Je, unaamini hilo? Unafikiri unaweza kusema na Mwamba? Je, unataka kuzungumza Naye, kwa ajili ya ugonjwa wako wa kisukari, sasa hivi? Simama kwa miguu yako basi. Hiyo ni kweli? Sema tu, "Ninamkubali Yesu Kristo sasa kama mponyaji wangu," naye Mungu atakupeleka nyumbani na kukupa afya. Nena na Mwamba. Mungu akubariki. Vema. Nenda ukaponywe.

<sup>223</sup> Unaonaje kuhusu hilo, unayeketi karibu naye, mama? Una mishipa iliyovimba miguuni mwako, sivyo? Hiyo ni kweli. Simama kwa miguu yako. Huyu si ni mumeo anayekaa karibu nawe hapo? Hiyo ni kweli? Una kisukari pia, sivyo? Je, hiyo ni kweli? Weka mkono wako juu ya mke wako. Vema. Nyote wawili mnatoka Illinois. Hiyo si ni kweli? Sasa wewe rudi Illinois, unene na Mwamba, nao utakuacha wala hautarudi tena. Haleluya!

<sup>224</sup> Ninajua jambo moja, ya kwamba Mwamba uko hapa, Mwamba wa Miaka uliopigwa nyikani. Hiyo ni kweli.

<sup>225</sup> Unaonaje juu yake, maskini mama hapo uliye na hayo maua kwenye kofia yako? Ukiketi hapo na ugonjwa wa yabisi kavu, ukijaribu kuuondokea. Wewe uliyegeuka na kuangalia upande mwingine, unaamini kwa moyo wako wote kwamba Mungu atakuponya? Simama kwa miguu yako basi, na kuchapua miguu yako juu-chini, na kusema, "Yabisi kavu imekwisha," na ndivyo ilivyo. Nena na Mwamba, Naye ataoa...?...

<sup>226</sup> Nawaambia, Yesu Kristo ni yeye yule jana, leo na hata milele. Yuko hapa kudhihirisha chochote ambacho... .

<sup>227</sup> Unaonaje kuhusu hilo, mama uliyeketi hapo, uliyesema, "Bwana asifiwe," mwenye shida hiyo ya kike, uliyevalia koti dogo la kijani kibichi, unayeketi hapo? Je, unaamini ya kwamba Mungu alikuponya basi? Simama, kwa dakika moja tu; unayeketi papo hapo. Je, unaamini kwa moyo wako wote? Una shida ya kike. Ni usaha. Una kifereji, namna fulani ya mtiririko hutoka humo. Hiyo si ni kweli? Ikiwa hiyo ni kweli, inua mkono wako. Ni kitu gani kinachonifanya niseme hivyo? Ni Mwamba akisema nawe. Mjibu, upate kuponywa. Haleluya!

<sup>228</sup> Loo, jinsi anavyotaka kuleta madhihirisho Yake ya nguvu Zake! Nami ninamwona Malaika wa Mungu, Nguzo ile ile ya Moto iliyowafuata wale wana nyikani, ikipitia kwenye jengo hili sasa.

<sup>229</sup> Ninajaribu kumtafuta mwanamke fulani. Anaomba. Yuko wapi hapa? Huyu hapa amesimama. Naam, ni maskini mwanamke anayesimama papo hapo, wa pili aliyeketi humo.

Hapana, yeye...Ni kuhusu mwanamume, aliyesimama. Ni mume mlevi unayemwombea. Hiyo si ni kweli, mama? Kama ni kweli, simama kwa miguu yako papo hapo. Si una mume mlevi uliyekuwa ukimwombea? Kama hiyo ni kweli, inua mkono wako. Nena na Mwamba, na Mungu atamtoa kutoka kwenye—kwenye jambo hilo.

<sup>230</sup> Mungu atafanya lolote hapa ndani, kama tu utalitenda. Je, unaamini hilo? Je, unaweza kuzungumza na Yeye? Ikiwa unaweza, simama kwa miguu yako sasa hivi na unene na Mwamba, nao Mwamba, utatoa maji Yake. Je, utasimama?

<sup>231</sup> Ni nani anayemtaka kwa ajili ya wokovu? Inua mkono wako, useme, “Ninamtaka aingie moyoni mwangu.” Mungu akubariki. Mungu akubariki. Mungu akubariki. Mungu akubariki, na wewe, na wewe, na wewe. Loo, jamani! Naam, bwana.

<sup>232</sup> Hiyo kansa ilikuacha hapo, ndugu yangu. Imekwisha. Unaweza kwenda nyumbani na kuwa mzima sasa. Haleluya! Hiyo ni kweli.

<sup>233</sup> Wote wanaotaka kuponywa, inua mkono wako, useme, “Bwana, ninasema Nawe. Ninasema Nawe.” Hiyo ni kweli.

<sup>234</sup> Huyu hapo anaenda. Bwana, mapindi yako yalikuacha pale. Uko huru. Nenda nyumbani; katika Jina la Yesu Kristo, umepona.

<sup>235</sup> Mtu yeyote hapa ndani, anayetaka kumpata sasa, inua mikono yako useme, “Asante, Bwana, kwa kuniponya. Ninasema Nawe, katika Jina la Yesu Kristo, kwamba uniponye.”

<sup>236</sup> Ee Mungu, wa rehema, tuma nguvu Zako usiku wa leo, pamoja na upako wa Roho Mtakatifu, wakati Yeye akiwa katika jengo hili sasa, apate kupitia kwa wasikilizaji hawa. Na jalia Roho Mtakatifu afanye kila muujiza. Jalia kusiwe na mgonjwa ama kiwete aliyesalia humu jengoni usiku wa leo. Naomba umponye kila mtu, katika Jina la Yesu Kristo.



*UKOMBOZI KATIKA UKAMILIFU, KATIKA FURAHA* SWA54-0330

(Redemption In Completeness, In Joy)

Ujumbe huu uliohubiriwa na Ndugu William Marrion Branham, uliotolewa hapo awali katika Kiingereza Jumanne jioni, tarehe 30 Machi, 1954, kwenye Kanisa la Mlango Uliofunguliwa huko Louisville, Kentucky, Marekani, umetolewa kwenye kanda ya sumaku iliyorekodiwa na kuchapishwa bila kufupishwa katika Kiingereza. Tafsiri hii ya Kiswahili ilichapishwa na kusambazwa na Voice Of God Recordings.

SWAHILI

©2022 VGR, ALL RIGHTS RESERVED

VOICE OF GOD RECORDINGS

P.O. Box 950, JEFFERSONVILLE, INDIANA 47131 U.S.A.

[www.branham.org](http://www.branham.org)

## Ilani ya haki ya kunakili

Haki zote zimehifadhiwa. Kitabu hiki kinaweza kuchapishwa kwa matbaa ya nyumbani kwa matumizi ya kibinafsi ama kusambaza, bila malipo, kama chombo cha kuitangazia Injili ya Yesu Kristo. Kitabu hiki hakiwezi kikauzwa, kunakiliwa kwa wingi, kuwekwa kwenye mtandao, kuhifadhiwa kikatolewe tena, kufasiriwa katika lugha zingine ama kutumiwa kuomba fedha bila idhini halisi iliyoandikwa moja kwa moja kutoka Voice Of God Recordings®.

Kwa habari zaidi ama kwa vifaa zaidi, tafadhali wasiliana na:

VOICE OF GOD RECORDINGS  
P.O. Box 950, JEFFERSONVILLE, INDIANA 47131 U.S.A.  
[www.branham.org](http://www.branham.org)